لجنة توزيع المطبوعات الدينية على الحجاج والمعتمرين

# MUONGOZO WA MWENYE KUFANYA IBADA YA HIJJAH NA UMRA


KIMEKUSANYWA NA KUANDALIWA NA

**SHEIKH TWALAAL BIN AHMAD AL- AQIIL**

Kimefasiriwa na

**Shahidu Mohamed na Abdullahi Abdi**




- Miiqat za kuhirimia
- Namna ya kufanya Umra
- Siku ya tarehe nane
- Siku ya Arafa
- Muzdalifa
- Siku ya kuchinja
- Masiku ya Tashriiq
- Hukmu zinazo muhusu muumini wa kike
- Fat-wa muhimu
- Msikiti wa Mtume
- Duwa zilizo chaguliwa


KIMEPITIWA NA SHEKH

**WAZIRI WA MAMBO YA KIISLAMU NA DA`AWA NA UELEKEZAJI**

# MUONGOZO WA MWENYE KUFANYA IBADA YA HIJJAH NA UMRA

KIMEKUSANYWA NA KUANDALIWA NA
**SHEIKH TWALAAL BIN AHMAD AL- AQIIL**
Kimefasiriwa na
**Shahidu Mohamed na Abdullahi Abdi**



KIMEPITIWA NA SHEKH

**WAZIRI WA MAMBO YA KIISLAMU NA DA`AWA NA UELEKEZAJI**

# REJEA ZA KISHARIA


- Kitabu : ATTAHQIIQ WAL-IDHWAAH. Cha sheikh Abdul-aziz Bin baaz
- Kitabu : SWIFATUL-HAJJ WAL-UMRA. Cha sheikh Muhammad Bin Swaleh Bin Uthaimin
- Kitabu :: AHKAMUN TAKHTASSU BIL-MU`MINAAT. Cha Dr.Swaleh Bin Fauzaan Alfauzaan .
- Kitabu : HISNUL-MUSLIM. Cha Sheikh Sai`d Bin Wahfu Alqahtwaaniy
- Kitabu : FATAWAL-LAJNA ADDAAIMAH



ⓗ طلال بن أحمد العقيل، ١٤٢٣هـ

فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر

العقيل، طلال بن أحمد

دليل الحاج والمعتمر، - جدة،

٨٠ صفحة ، ١٢ x ١٧ سم

ردمك: ٩-٩٦٤-٤١-٩٩٦٠

١ - الحج - مناسك    ٢ - العمرة    أ - العنوان

ديوي ٢٥٢,٥    ٢٣/٣٩١٧

رقم الإيداع: ٢٣/٣٩١٧

ردمـــــك: ٩-٩٦٤-٤١-٩٩٦٠



حقوق الطبع محفوظة



هاتف: ٦٣٩١٨٠٠ - فاكس: ٦٩٨٦٣٥٥ - جوال: ٠٥٥٦٤٨٦٥٩

ص . ب: ١٨٤٥٥ - جـدة ٢١٤١٥

المملكة العربية السعودية

أعوذ بالله من الشيطان الرجيم

ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا
فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ
ٱللَّهُۗ وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُوْلِي
ٱلۡأَلۡبَٰبِ ١٩٧ لَيۡسَ عَلَيۡكُمۡ جُنَاحٌ أَن تَبۡتَغُواْ
فَضۡلٗا مِّن رَّبِّكُمۡۚ فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ
فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا
هَدَىٰكُمۡ وَإِن كُنتُم مِّن قَبۡلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ١٩٨
ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَۚ
إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ١٩٩ فَإِذَا قَضَيۡتُم مَّنَٰسِكَكُمۡ
فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَذِكۡرِكُمۡ ءَابَآءَكُمۡ أَوۡ أَشَدَّ ذِكۡرٗاۗ
فَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِي ٱلدُّنۡيَا وَمَا لَهُۥ
فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنۡ خَلَٰقٖ ٢٠٠ وَمِنۡهُم مَّن يَقُولُ رَبَّنَآ ءَاتِنَا
فِي ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ حَسَنَةٗ وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ٢٠١
أُوْلَٰٓئِكَ لَهُمۡ نَصِيبٞ مِّمَّا كَسَبُواْۚ وَٱللَّهُ سَرِيعُ ٱلۡحِسَابِ ٢٠٢

# UTANGULIZI

Shukurani zote zinamsitahiki Allah, ambae kawafaradhishia wenye uwezo miongoni mwa waja wake ,kwenda kuhiji katika nyumba ya Allah tukufu,na akaijaalia Hijjah iliyokubaliwa ni sababu ya kufutiwa na kusamehewa madhambi na makosa, swala na salamu zimwendee Mtume wetu Muhammad ambae ni mteuliwa, mbora wa waliotufu na kufanya Saayi, na Mtukufu wa waliofanya Talbiya na kuomba, na sala na salamu ziwaendee pia ahali wake na maswahaba wake, na watakao wafuata kwa wema na Wakawaiga, Amma baad.

Hakika mimi nakukaribisha ewe ndugu yangu ulie kuja katika ibada tukufu ya Hijjah,katika viwanja vya mji huu wa amani,na namuomba Allah alie takasika na kutukuka akufanyie wepesi wa kutekeleza ibada hii ya Hajji na Umra kwa namna ambayo Inamridhisha, na aifanye ibada yako hii ni kwa ajili ya kutafuta radhi zake tu, na iwe yenye kufuata muongozo wa Mtume, na aikubali ibada yako na aiweke katika mizani ya mema yako.

Ndugu yangu mpendwa ulie ikusudia nyumba tukufu ya Allah..Ikiwa kila msafara huwa unakuwa na kiongozi, na kila safari lazima iwe na muelekezaji, basi tambua kwamba kiongozi wa msafara wa mahujaji ni Mtume Muhammad -swala na salamu zimwendee- na muelekezji wao ni muongozo wake Mtume na suna zake, na Yeye ndie aliyesema:

***" CHUKUENI KWANGU UTARATIBU WA IBADA YENU YA HIJJAH"***

Kwahiyo imekuwa ni lazima kwa kila mwenye kuikusudia nyumba ya Allah kwa ajili ya ibada ya Hijja au Umrah, ajifunze mwongozo wa Mtume katika ibada hiyo kupitia vitabu sahihi vinavyo fundisha ibada hiyo, pia awaulize wenye elimu katika yale yatakayo mtatiza..

Na mbele yako ewe ndugu yangu mwenye kuiendea ibada ya Hijjah, hiki ni kitabu ambacho ibara zake ni nyepesi kabisa, chenye muundo mpya, kinakufafanulia hukmu za Hijjah na Umra, kwa ibara zilizo wazi, na vielelezo vyenye kubainisha, ni matarajio yangu kuwa utakifanya ni muongozo wako katika Hijja yako na Umra yako, ikiwa litakutatiza jambo lolote, basi Wizara ya mambo ya kiislamu nchini Saudi Arabia inafuraha kubwa kukuhudumia katika kukubainishia kila unacho kihitajia, maana imeandaa vituo, na vibanda maalumu ambavyo

# UTANGULIZI

utawakuta humo wanazuoni watakao kuelekeza kwa kila unacho kihitajia katika maarifa, na hii ni kutekeleza agizo la Allah aliposema :

فَسۡـَٔلُوٓاْ أَهۡلَ ٱلذِّكۡرِ إِن كُنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ ﴿٧﴾ الأنبياء

***"Waulizeni wenye kujua ikiwa ninyi hamjui "*** Al-anbiyaa : 7
Mwisho kabisa napenda nitoe shukrani zangu nyingi kwa ndugu yangu Shekh Twalaal Bin Ahmad Al-aqiil aliye andaa muongozo huu. Namuomba Allah aujaalie muongozo huu pamoja na juhudi zake nyingine anazo zitoa katika Nyanja hizi, ajaalie ni katika mizani ya mema yake, na Allah amzidishie malipo yake ,yeye pamoja na wenzie katika kitengo cha kugawa vipeperushi na machapisho ya muongozo kwa mahujaji na wanao kuja kufanya Umra kupitia hapa Jiddah kutokana na kazi yao kubwa hii ambayo ni yenye kubarikiwa inshallah.

Na kama kuna wasia wa kukupa ewe uliekuja ni mgeni katika nyumba ya Allah,basi nakuusia na kuiusia nafsi yangu katika kuutumia vizuri muda huu wa thamani katika kufanya yale yatakayo kupatia radhi za Yule ambaye umekuja ukiwa ni mgeni wake,na umefikia katika mipaka ya nyumba yake tukufu, pia nakuusia uyaache yote ambayo yanayo mchukiza,na anayo yakataza, maana Allah Amesema :

وَمَن يُرِدۡ فِيهِ بِإِلۡحَادِۭ بِظُلۡمٖ نُّذِقۡهُ مِنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ﴿٢٥﴾ الحج

" Na yeyote atakaye kusudia kuchupa mipaka kwa kufanaya dhulma katika Haram,basi tutamuonjesha adhabu iumizayo " Alhajj : 25
Namuomba Allah aijaalie Hijjah yako ni yenye kukubaliwa,na juhudi zako ziwe zenye kushukuriwa,na madhambi yako yawe ni yenye kusamehewa.
Na Allah ndie mjuzi zaidi.
Sala na salamu zimwendee mja wake na Mtume wake, kiongozi wetu,na kiigizo chetu na kipenzi chetu Muhammad,pamoja na Ahli wake na Maswahaba wake na wafuasi wake.
Wassalaamu Alaykum warahmatullahi wabarakaatuh.

**Waziri wa maswala ya Kiislamu na Da`awa na uelekezaji**

# QIBLA CHA WAISLAMU

Ndiko zinako elekea nyoyo za Waislamu wote popote walipo duniani ,katika nyumba hii nyuso zote zinaelekea pamoja na nyoyo , katika hali ya kunyenyekea na kumdhalilikia Allah mmoja wa pekee, mara tano kila siku usiku na mchana..

Na wanamiminika Waislamu katika nyumba hii kongwe kutoka kila upande wa dunia,ili watekeleze ibada zao,na ili wafanye twawafu katika Alkaaba tukufu, tangu alipoijenga kipenzi wa Allah Nabii Ibrahim, na ikawa Alkaaba ndiyo nyumba pekee iliyowekwa kwa ajili ya watu ili wamuabudu Allah katika nyumba hiyo,kwa mungozo maalumu na kwa ujuzi,na kwa itikadi iliyo safi kabisa, iliyo salimika na itikadi batili na uelewa ulio batili.
Allah amesema :

إِنَّ أَوَّلَ بَيۡتٖ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكٗا وَهُدٗى لِّلۡعَٰلَمِينَ ٩٦
فِيهِ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٞ مَّقَامُ إِبۡرَٰهِيمَۖ وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنٗاۗ وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ
ٱلۡبَيۡتِ مَنِ ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٩٧

سورة آل عمران

***“ Hakika nyumba ya kwanza waliyo wekewa watu{ kufanya ibada} ni ile iliyoko Bakkah( MjiwaMakauliobarikiwa)iliyo barikiwa,na ndio muongozo kwa walimwengu wote. Ndani yake mna ishara zilizo wazi masimamio ya Ibrahim,na mwenye kuingia humo huwa katika Amani. Na kwa ajili ya Mwenyezi mungu imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo , kwayule awezae njia ya kwendea. Na atakayekanusha basi Mwenyezi mungu si mhitaji kwa walimwengu “*** . Aal-imraan : 96

## Amesema Mtume – Sala na salamu zimwendee- kwamba:

" Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano:

Na hapa inatubainikia kuwa Hijjah ni nguzo miongoni mwa nguzo za Uislamu..na kwamba haukamiliki Uislamu wa Mtu ambaye ni mwenye uwezo wa kwenda Hijjah mpaka atakapo hijji..

Lakini miongoni mwa neema za Allah kwetu ni kwamba Ameijaalia ibada ya Hijja ni wajibu mara moja tu katika umri wa mtu, kwasababu pindi Allah alipofaradhisha Hijjah,mtu mmoja akauliza: Je ni kila mwaka ewe Mtume wa Allah?? Hapo Mtume wa Allah akasema: " …Hijjah ni mara moja, atakayezidisha basi hio ni khiyari" Hadithi sahihi.

Na nilazima Hijjah iwe ni kwa ajili ya Allah tu,na isichanganyike na riyaa (kujionyesha),au kutaka kuskika na kutambulika, kwasababu Allah Amesema katika hadithil-qudsi:

" Mimi ni mwenye kujitosheleza nisie hitajia ushirika, mwenye kutenda amali yoyote ile akanishirikisha na mwingine,basi nitamuacha na ushirika wake".

Pia inatakikana Hijjah iwe ni yenye kuafikiana na mafundisho ya Mtume – Sala na salamu zimwendee-, na kwa ajili hiyo tunawausia ndugu zetu wanao kusudia kuja katika kutekeleza Ibada ya Hijjah kwamba: Kabla ya kufunga safari ya kuja katika Ibada hii kwanza wajifunze namna gani alivyo hiji Mtume-sala na salamu zimwendee-? Ili wapate kumuiga na kufuata maelekezo yake pale aliposema :

**" Chukueni kwangu mimi utaratibu wa Ibada yenu ya Hijjah "**

(Muslim)

- **Kushuhudia kwamba hapana apasae kuabudiwa kwa haqi ispokuwa Allah,na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.**
- **Kusimamisha swala tano**
- **Kutoa zaka**
- **Kufunga Ramadhani**
- **kuhiji katika nyumba tukufu ya Allah**

# MIONGONI MWA ADABU ZA SAFARI

1. Yampasa mwenye kutekeleza Ibada ya Hijjah au Umra akusudie kwa Ibada yake hiyo radhi za Allah , na kujikurubisha kwake,na atahadhari sana asijekuwa anakusudia maslahi ya kidunia,au kutafuta ufahari, na kutafuta jina,au utajo.

2. Ni sunna kwa mtu anapotaka kusafiri aandike wasia wake,abainishe haki za watu na haki zake zilizoko kwa wtu, na arejeshe amana za watu,au awatake idhini maalumu kuwa zibakie kwake,maana ajali ya mtu iko mikononi mwa Allah.

3. Atubie kutokana na Madhambi yake na maasi yote,na awe mwenye kuyajutia yaliyopita katika madhambi yake, na aweke azma ya kuto yarejea tena.

4. Arejeshe vitu ambavyo kawadhulumu watu,ikiwa ni mali,na kama ni kuwavunjia watu heshma zao basi akawaombe msamaha.

5. Achague kwa ajii ya safari yake hii chumo lililokuwa zuri la halali,kwasababu Allah ni mzuri kwahiyo hakubali ispokuwa vilivyo vizuri.

6. Ajiweke mbali na maaswi yote,na asimuudhi yoyote kwa ulimi wake,wala kwa mkono wake,wala asisababishe msongamano kwa mahujaji , msongamano ambao utawaletea maudhi au madhara,wala asijiingize katika utetaji na usengenyaji,wala asifanye mijadala ispokuwa kwa njia nzuri,wala asiseme uongo,wala asimsemee Allah jambo ambalo hana ujuzi nalo.

# MIONGONI MWA ADABU ZA SAFARI

7. Ni jukumu la mwenye kutaka kufanya ibada ya Hijjah au Umra ajifunze hukumu za Hijjah na Umra.

8. Ajitahidi sana msafiri kuchunga mambo yote ya wajibu,na miongoni mwa wajibu mkubwa ni Swala,aiswali ndani ya wakati wake kwa jamaa,na akithirishe mambo ya twaa,kama kusoma Qur-ani,kufanya Dhikri, kuomba dua, Kuwafanyia ihsani watu, kwa maneno na vitendo, na kuwasaidia wenye haja, na kuwa mpole kwa Waislamu wenzake, na kuwapa msadaka mafakiri, na kuamrisha mema na kukataza mabaya.

9. Ni vizuri msafiri ajitahidi kuchagua watu walio bora na wema ndio asafiri nao.

10. Msafiri ajipambe na tabia njema,hii inajumuisha kuwa na subra,kusamehe,kuwa mpole,kuwa na huruma, kutokuwa na haraka katika hukmu, kuwa mnyenyekevu, mkarimu,muadilifu,muaminifu, msamehevu,kuwa na haya, mkweli, mwenye ihsani.

11. Inapendeza kwa msafiri awausie watu wake kumcha Allah,na huu ni wasia wa Allah kwa nyumati za mwanzo na sisi ambao ni wa mwisho.

12. Inapendeza kwa msafiri adumu na dua na adhkari zilizopokewa kwa Mtume –Sala na salamu zimwendee- ikiwa ni pamoja na dua ya safari,dua ya kupanda kipandwa.

Ukurasa 78.

## MATENDO YA MWANZO YA HIJJAH NA UMRAH:

Na inakuswudiwa nia ya kuingia katika ibada, na muda wake ni wakati wowote kuwa mwaka mzima , na katika ibada ya hijjah itakuwa ni katika miezi ya hijjah ambayo ni:-

**Shawal , Dhul-qadah, na masiku kumi ya mwanzo katika mwezi wa Dhul-hijjah.**

Na zinaanza nguzo za hijjah na Umrah wakati mtu anapohirimia katika miqat ….

Atapofika mwenyi kukusudia Hijjah au Umrah katika miiqati , eidha amekuja kwa njia ya gari na mfano wake, inapendeza kwake aoge ajitie manukato ikiwezekana, na kama hakuoga pia sio vibaya, kisha avae ihram , mashuka miwili meupe masafi, na kwa mwanamke hana vazi maalum la ihram bali Anavaanguo yoyote yenye kuistiri mwili wake ya rangi yoyote isiyo dhihirisha mapambo,

kisha ananuwiya Umrah au Hijjah kwa kusema hivi:

Mwenye kufanya Umra atasema hivi :
**Labaika Umratan**

Mwenye kufaya Tamatu'u , atasema hivi :
**Labaika Umratan mutamatian bihaa ilal hajji.**

Mwenye kufanya Qiraan atasema hivi:
**Labaika Umratan wa Hajjan.**

Mwenye kufanya Ifrad atasema hivi :
**Labaika Hajjan**

**Na anapoanza kufanya talbiyyah anakuwa amekwisha tangaza kuingia katika ibada.**

Ama ikiwa amekuja kwa njia ya baharini au angani, imekuwa mara nyingi marubani wa ndege na manahodha wa Meli wanawatangazia wasafiri kwamba wanakaribia Miiqaati ili wajiandae kuvaa ihram, na wanapokuwa kwenye usawa wa Miiqaat wananuwiya Hajji au Umrah na wanakithirisha talbiyyah.

Na katika hali kama hii siovibaya kwa mtu akatoka nyumbani kwake katika nchi yake akiwa amevaa ihram. Kisha anaanza kufanya talbiya kama ishara ya kuingia kwake katika ibada pale anapojulishwa kwamba wamepita miiqaat au wako usawa na miiqaat.

Mwanaume atafanya talbiya kwasauti ya juu na sio mwanamke.

## QABLA YA IHRAM FANYA YAFUATAYO:

1. kukata kucha na kupunguza sharubu na kuondowa nywele za kwapa na za chini.
2. Kuoga mwili mzima ikiwezekana na asipooga hakuna ubaya nakuooga ni sunnah kwa wanaume na wanawake hata walio katika siku zao.
3. Mwanaume atavua nguo zilizoshonwa na atavaa ihram.
4. Mwamuke atavua niqab na glovsi …….. na atavaa mtandio ili apate kufunika uso wake na kichwa chake wakati akipishana na wanaume ambao sio maharim zake na hata kama mtandio utagusa uso wake hakuna ubaya.
5. Baada ya kuoga mwanaume atajipaka manukato mwilini tu, wala asipake ihram.

**Mwanamke atajipaka manukato yasio dhihirisha harufu yake .**

6. Baada ya kumaliza kufanya yaliyotajwa ananuwiya kuingia katika nusuki anayoitaka, akinuwia kuingia katika nusuki kwa kufanya hivyo anakuwa amekwishahirimia hata kama hakutamka chochote, na akifanya niya yake ikawa baada swala ya faradhi ni viziri zaidi. Na ikiwa sio muda wa swala ya faradhi akaswali rakaa mbili za sunnah ya udhu sio vibaya. Na kama anamuhijia mtu au anamfanyia umrah basi atanuwiya kwa niaba yake aseme : Labaika Allahuma an ……. Kisha amtaje .

Ihram haina salah maalum

**NAMNA YA KUFANYA TALBIYAH:** ( Labaika Allahuma labbaika , labbaika laa sharika laka labaika, innal-hamda wa-niimata laka wal-mulk laa sharika laka) .

**MUDA WA KUFANYA TALBIYAH:** Katika ibada ya umrah ni tangu anapohirimia mpaka atakapoanza kutufu . Katika ibada ya hijjah ni tangu anapohirimia mpaka atakapo tupa mawe (jamarati) asubuhi ya siku ya idi.

# VITUO VITANO VYA KUHIRIMIA

Mtume –Sala na salamu zimwendee - ameainisha vituo vitano kwa ajili ya kuhirimia (kunuwia) Hijjah au Umra. kwahivyo ni lazima kwa kila anayekusudia ibada ya Hijja au Umra atie nia katika mojawapo ya vituo hivyo vitano.

Na vituo vyenyewe ni hivi:

| | |
|---|---|
| **DHUL HULAIFAH** | Ni miiqat ya watu wa Madina ,na kila atakaye kuja Makkah kupitia njia hiyo, na Miiqat hii kwa sasa inajulikana kwa jina hili ABYAARU ALY, ni umbali wa km 450 kufika Makkah. |
| **AL -JUHFA** | Ni miiqat ya watu wa Shamu,Moroco,Misri na kila atakaye kuja Makkah kupitia njia hiyo, Miiqat hii iko karibu na mji wa Raabigh,na watu siku hizi wanahirimia hapo Raabigh. Ni umbali wa km 183 kufika Makkah |
| **QARNUL-MANAAZIL:** | Ni Miiqati ya watu wa Najdi,na kila atakaye kuja Makkah kupitia njia hiyo . Na kwa sasa inaitwa AS-SAILUL-KABIIR. Ni km 75 kufika Makka |
| **YALAMLAM:** | Ni miiqati ya watu wa Yaman, na kila atakae kuja Makkah kupitia njia hiyo. Na kwa sasa watu wanahirimia sehemu iitwayo Assaadiyyah, ni km 92 kufika Makkah. |
| **DHAATU IRQI :** | Ni Miiqati ya watu wa Iraki, na kila atakayekuja Makkah kupitia njia hiyo. Ni km 94 kufika Makkah. |

Hiyo ni wajibu kwa kila atakayepita katika Miiqati hizi na akawa anakusudia Hijjah au Umra ahirimie hapo katika Miiqati hizo..na atayezivuka makusudi bila ya kuhirimia itamlazimu kurejea katika Miiqati hizo ili akahirimie, na kama hakufanya hivyo basi inamlazimu damu , yaani achinje mnyama kwa kosa hilo , kisha aigawe nyama hiyo kwa mafakiri wa Makkah.

# VITUO VITANO VYA KUHIRIMIA

Amesema Mtume – Sala na salamu zimwendee- kwamba: " Miiqati hizo ni za watu wa maeneo hayo,na kila atakepitia katika maeneo hayo akiwa sio miongoni mwa watu wa maeneo hayo, miongoni mwa wanao ikusudia Makkah kwa ajili ya Hijjah au Umra "

Imepokelewa na Bukhari na Muslim .

- Na kwa watu wa Makkah- kadhalika watakao kuwa Makkah ambao sio wakaazi wa hapo- wao watahirimia palepale Makkah kwa ibada ya Hijjah,ama kwa ibada ya Umra wanatakiwa wakahirimie nje ya mipaka ya Haram,kama vile TAN`IIM.
- Ambao makazi yao wako ndani ya miqaat kama wakazi wa maeneyo yafatayo :-

| | |
|---|---|
| Jeddah | Bahrah |
| Masturah | Umm Salim |
| Badr | Al-Shae' |

Watu hawa watahirimia majumbani mwao , au sehemu yoyote ilipowajia nia ya Hajji au Umrah.



# YANAYO KATAZWA BAADA YA KUHIRIMIA



Bada ya kuhirimia katika miiqaat ni haraam mwenye kufanya Hijjah na Umrah Mambo yafuatayo :



- Kuondoa chochote katika nywele au kucha, lakini endapo kitatoka chenyewe bila kukusudia,au akifanya hivyo kwa kusahau au bila kujua hukmu atasamehewa.



- Haifai kwa mwenye kuhirimia kutumia manukato katika mwili au nguo, lakini sio vibaya akipatwa na athari ya manukato aliyotumia kabla ya kuhirimia ama yakimpata katika nguo yake lazima aioshe.





- Haifai kwa mtu aliyehirimia kufunika kichwa kwa ihram na Hata kwa kitu kingine kinachovaliwa kichwani kama kofia , kiremba na mfano wake. Na endapo mtu atafunika kichwa chake kwa kusahau au kwa kutokujua hukmu, inamlazimu akiondoe kitu hicho pale atakapo kumbuka au akajua hukmu, na wala hatawajibikiwa na chochote.



- Haifai kwa mwenye kuhirimia kuvaa nguo iliyoshonwa, katika mwili wote au sehemu ya mwili, kama kanzu, shati, fulana, suruwali, khofu. Ispokua kama hakupata ihram inafaa kuva suruwali, na ambaye hakupata ndala inafaa kuva khofu wala hakuna ubaya.
- Haifai kwa mwenye kuhirimia kuposa, na kufunga ndoa sawasawa iwe yakwake au ya mwingine, na kufanya

# YANAYO KATAZWA BAADA YA KUHIRIMIA







tendo la ndoa na kugusana na mwanamke kwa matamanio, kutoka na hadithi ya Uthman - Radhi za Allah zimwendee – kwamba Mtume – Salamuza Allah zimuendee – Amesema : ( Sio ruhusa kwa mtu ambaye yuko katika ihram kuoa, wala si ruhusa kuolewa, wala si ruhusa kuchumbia ). Imepokewa na muslim.

- Si ruhusa kwa mwenye kuhirimia katika kipindi cha ihram kuvaa glovsi na kufunika uso wake kwa niqab. Ama akiwa mbele ya wanaume ambao siyo maharim zake wakati huo ni lazima astiri uso wake kwa mtandio au kitu chochote mfano wake. Kama anavyo wajibika kufanya hivyo pindi anapokuwa katika hali isiyokuwa ya Kuhirimia.

- Haifai Kwamuislamu akiwa amehirimia au hakuhirimia kuokota chochote kama pesa, Dhahabu, Fedha na viti vingine katika Mji mtukufu wa Makkah ispokua kwa nia ya kuvitangaza.

- Haifai kwa muislami akiwa amehirimia au hakuhirimia ,mwanaume au mwanamke kuwinda viwindwa vya nchi kavu au kuvifukuza au kumsaidia mtu katika hilo ndani ya mipaka ya haram ……. Na mtu mwenye kuhirimia haruhusiwi kufanya hivo ndani na nje ya mipaka ya haram.

- Ni haramu kwa muislamu ikiwa amehirimia au ha kuhirimia kukata mti wa haram na mimea yake ya kijani nyenye kujiotesha nyewe.

## ANARUHUSIWA MWEYE KUHIRIMIA MAMBO YAFWATAYO



- Kuvaa pete
- Kuvaa saa
- Kuvaa ndala
- Kuvaa kifaa cha kusikilizia
- Kutumia mwanvuli
- Kuvaa miwani
- Kupanda gari
- Kuvaa mkanda
- Kufunga jiraha
- Kuosha kichwa hata kama zitatoka baadhi ya nywele bila kukusudua hakuna ubaya

- **Na anaruhusiwa mwenye kuhirimia :**
- Kubeba vitu kichwani
- Kubadelisha ihram, na endapo atafunika kichwa chake kwakusahau au bila kujua hukmu anawajibika ukiondoe maramoja hicho kilichofunika bada ya kukumbuka au bada ya kujua hukmu, wala hawajibikiwi na chochote.

# NUSUKI TATU

Inamlazimu kila mwenye kutaka kufanya Ibada ya Hijjah achague moja kati ya hizi nusuki tatu:

Nusuki iliyo bora kati ya hizi tatu ni Tamatui

| | |
|---|---|
| **1 TAMATTUI**<br>**Umrah**<br>**Hajj**<br>**Hadi** | Utaratibu wake ni Kuhirimia Umra ndani ya miezi ya Hijjah ambayo ni Shawwaal,Dhul-qaadah na masiku kumi ya mwanzo ya mwezi wa Dhulhijjah,anasema (LABBAIKA UMRATAN MUTAMATTIAN BIHAA ILAL-HAJJI), anafanya Twawaafu na Saayi kisha anapunguza nywele zake. Na hapo anakuwa kamliza Umra, anakuwa huru, mpaka itakapofika tarehe nane ya mwezi wa Dhul-hijjah,atahirimia Hijjah pale alipo,kisha anaelekea katika maeneo husika ya Ibada ya Hijjah kwa ajili ya kukamilisha ibada yake, na anawajibikiwa kuchinja mnyama,eidha mbuzi au kondoo,au ng`ombe mmoja kwa watu saba, au ngamia mmoja kwa watu saba pia,kama hakupata basi analazimika kufunga siku tatu ndani ya masiku ya Hijjah na siku saba akisharudi nchini kwake,jumla zinakuwa siku kumi. |
| **2 QIRAAN**<br>**Umrah**<br>**Hajj**<br>**inamlazimu kichinjwa** | Utaratibu wake ni : Kuhirimia Umra na Hijjah kwa pamoja kwa kusema : (LABBAIKA UMRATAN WA HAJJAN ), akifika Makkah anatufu twawafu ya kufika,kisha anafanya Saayi ya Hijjah pamoja na Umra (Yaani hizo raundi saba zinakuwa kwa niaba ya Hijjah na Umra), na atabakia katika Ihramu yake,kisha siku ya tarehe nane anatoka kuelekea katika viwanja vya ibada ya Hijjah ili kukamilisha matendo yaliyo salia ya Ibda ya Hijjah,ispokuwa nikwamba hatofanya tena Saayi,ile ya kwanza inamtosha. Kisha huyu inamlazimu kichinjwa, eidha mbuzi au kondoo,au ng`ombe mmoja kwa watu saba, au ngamia mmoja kwa watu saba pia,kama hakupata basi analazimika kufunga siku tatu ndani ya masiku ya Hijjah na siku saba akisharudi nchini kwake,jumla zinakuwa siku kumi. |
| **3 IFRAD**<br>**Hajj pekeyake**<br>**hawajibikiwi kichinjwa** | IFRAAD : Ambayo ni : Hijja pekeyake,na wala hawajibikiwi kichinjwa. Utaratibu wake ni : Kuhirimia Hijjah pekeyake,akifika Miiqat anasema : (LABBAIKA HAJJAN) ,na akifika Makkah anafanya Twawaaful quduum,na anafanya Saayi ya Hijjah, na anabakia katika ihraamu yake mpaka atakapokamilisha Ibada ya Hijjah, na wala hawajibikiwi kichinjwa kwasababu hakukusanya Ibada ya Hijjah na Umra ndani ya safari moja. |

Nusuki hii ndiyo ambayo Mtume- Sala na salamu za Allah zimwendee - aliwaamrisha Maswahaba waifanye

# FAIDA:

**Kuhirimia katika Miiqaat ni lazima kwa watu wote.**

**IFRAD**
**Yaani Hijjah pekayake**
↓
**Anatufu twaaf kufika**
↓
**Anafanya sai ya Hijjah**
↓
**atabakia katika ihramyake paka siku ya kuchinja, na anajiupusha na mambo yote yalikatazwa kwa mwenye kuhirimia.**

**QIRAN**
**Yaani Hijjah na Umrah**
↓
**Anatufu twaaf kufika**
↓
**Anafanya sai ya Hijjah na Umrah**
↓
**atabakia katika ihramyake paka siku ya kuchinja, na anajiupusha na mambo yote yalikatazwa kwa mwenye kuhirimia.**

**TAMATUU**
**Yaani Hijjah na Umrah**
↓
**Anatufu awaaf ya Umrah**
↓
**Anafanya sai ya umrah**
↓
**Ana punguza aw kunyowa nywele za kichwani.**
↓
**Anatoka katika ihram, na anahalalikiwa kila kitu katika vile aliviokwa amekatazwa hata wanawake, na anahirimia hijjah siku ya tarehe nane.**

1- Twawafu ya kufika kwa mtu anayekusudia kufanya nusuki ya Ifraad pia mwenye kufanya Qiraan ni Sunnah,kwahiyo wakiiacha hakuna lawama.

2- Pindi atakapo tufu twawafu ya kufika na akaelekea Mina moja kwa moja, baada ya ile twawafu ya Ifaadhwa atafanya Saayi ya Hijjah.

- Mtoto mdogo ambaye hajabalehge akiletwa hijjah basi walii wake ataweka nia kwa niaba yake,kisha atamvua nguo na kumvisha Ihraamu,na atafanya Talbia kwa niaba yake, kwa kufanya hivyo mtoto atazingazitwa yuko katika Ihraamu,kwahiyo atajizuwia na yale yote anayojizuwia nayo mtu mzima wakati wa Ihramu.
- Binti ambaye hajafikia umri wa kupambanua pia nae walii wake atamuwekea nia ya Ihraamu ,nae atazingatiwa yuko katika Ihraamu,na atajizuwia na mambo yote anayotakiwa kujizuia nayo mwanamke mtu mzima katika wakati wa Ihraamu.
- Inatakikana wakati wa kufanya twawafu wawe na twahara katika miili yao na nguo zao,maana twawafu ni kama swala, na twahara ni miongoni mwa masharti ya kusihi swala.

- Itakapokuwa Mtoto wa kiume na wa kike wote wamefikia umri wa kupambanua basi watahirimia wenyewe kwa idhini ya walii wao,na watafanya wakati wa kuhirimia yote anayoyafanya mtu mzima,kama kuoga,kutia manukato mwilini na kichwani kabla ya kuvaa ihram n.k

# MAARIFA YA IBADA YA UMRAH

***Amesema Mtume wa Allah –Sala na salmu za Allah zimwendee- :***

**" العمرة إلى العمرة كفارة لما بينهما و الحج المبرور ليس له جزاء إلا الجنة "**

**“ Kutoka Umra moja mpaka Umra nyingine ni sababu ya kufutiwa makosa na madhambi yaliyotendeka baina ya umra hizi mbili, na Hijjah ambayo ni Mabruu (iliyokubaliwa) haina malipo ispokuwa ni Jannah “.**



## TWAWAFU YA UMRA

**Pindi anapofika Makkah yule aliyekuja kwa ajili ya Umrah,**

ni Sunnah aoge mara tu baada ya kufika kwake,kisha baada ya hapo aelekee Msikiti mtukufu wa Makkah palipo na nyumba kongwe ya Allah,ili akatekeleze ibada ya Umrah. Na atakapokwenda katika Haramu bila ya kuoga hatakuwa na kosa. Na wakati wa kuingia katika Msikiti mtukufu wa Makkah atatanguliza mguu wake wa kulia na kusema:

***(AUDHUBILLAAHIL-ADHWIIM, WASULTWAANIHIL-QADIIM, MINASHAITWAANIR-RAJIIM, ALLAAHUMMAF-TAH LII ABWAABA RAHMATIKA ).***

***Kisha anaelekea mfanya umra:*** Panapo Al-kaaba tukufu ili akaanze Twawaafu, na ni katika Sunnah kwa wanaume kuvaa rubega wakati wa kutufu twawafu ya Umra na Twawafu ya kufika ( Twawaafulquduum) tu.

***Kisha anaanza mfanya Umra :*** Kutufu mara saba akianzia katika Hajarul-aswad, na kama ikimuwzekania kufika katika Hajarul-aswad basi atalibusu kama ataweza lakini pasina kuwaudhi watu kwa msongamano na kuwasukuma wala kutukanana na kupigana,maana kufanya hivyo ni makosa,maana kufanya hivyo ni kuwaudhi Waislamu. Na inatosha akaashiria upande wa Hajarul-aswad kwa mbali huku akisema: ***Allahu akbar*** bila ya kusimama.

Na haifai kusongamana na watu au kuwaudhi watu.

## TWAWAFU YA UMRA

**Kisha anaendelea katika raundi saba :**

Na ajiepushe kuwaudhi watu kwa msongamano na kunyanyua sauti, na aombe dua yoyote atakayo na kusoma Qur-ani,na atambue kwamba Twawafu haina dua maalumu kama wanavyofanaya baadhi ya watu.

**Kisha anaendelea katika raundi saba :**

Katika pembe inayoitwa ***(ALYAMAANIY)*** ni ile inayofuatana na Hajarul-aswad, basi atagusa hapo kwa mkono wake kama itamuwezekania,lakini hapo hakuna kubusu wala kujipangusa katika pembe hiyo kama wafanyavyo baadhi ya watu,hali ya kuhkalifu Sunnah ya Mtume. Na kama hakuweza kugusa hapo basi aendelee na twawaafu bila ya kuashiria hapo wala kupiga takbira. Na ni katika Sunnah aseme wakati akitufu pindi anapofika baina ya Ruknul-yamaani na Hajarul-aswd dua hii:

***(Rabbanaa aatinaa fid-duniyaa hasanatan, wafil-aakhirati hasanatan, waqinaa adhaaban-naar)***

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾

سورة البقرة (Qur-an 2:201)

**Ndio kama hivyo atakamilisha twawafu yake kwa utaratibu huu ,**

mpaka afikishe raundi saba, kila raundi anahesabu kuanzia katika Hajarul-aswad na kuishia hapo hapo. Na ni katika sunna anapofanya Twawaful-quduum na Twawafu ya Umra kwenye raundi tatu za mwanzo awe ni mwenye kukimbia kidogokidogo kwa hatua za karibukaribu ( kama mchakamchaka).

# KUTUFU RAUNDI SABA






**UNAANZIA KATIKA HAJARUL-ASWAD NA UNAMALIZIA HAPO**

# BAADHI YA MAKOSA WAKATI WA KUTUFU

- Baadhi ya watu wanatufu ndani ya Hijri (Eneo lililo upande wa ndani ya maqaamu Ibraahim) huku wakiitakidi kwamba twawaafu yao ni sawa,ilihali kwamba eneo hilo linazingatiwa ni ndani ya Alkaaba, kwahiyo nilazima mtu atufu upande wa nje.

- Kugusa kona zote za Alkaaba,wakati mwingine mpaka kuta zake, kisha hujipaka mwilini,au kujipangusa katika mlango wa Alkaaba,au katika Maqaamu Ibraahim. Mambo yote haya hayafai,maana ni katika uzushi ambao hauna asli kabisa katika Sharia,na Mtume wetu –Sala na salamu za Allah zimwendee- hakuyafanya.

- Wanawake kusongamana na wanaume wakati wa twawafu,hasa katika Hajarul-aswad na katika Maqaamu Ibraahim, inatakiwa wajiweke mbali sana na jambo hili.

**UNAANZIA KATIKA HAJARUL-ASWAD NA UNAMALIZIA HAPO**

1. Afunike bega lake la kulia .
2. Aswali rakaa mbili nyuma ya Maqaamu Ibraahim ikiwa itamuwezekania, na akishindwa basi aende sehemu yoyote ile hapo msikitini, na hizo rakaa mbili ni Sunnah iliyokokotezwa. Katika rakaa ya kwanza baada ya kusoma Suratil-faatiha atasoma :

سورة الكافرون

Suuratul-kaafiruun, na katika rakaa ya pili baada ya Suuratil-faatiha atasoma : Suuratul- ikhlaas.

سورة الإخلاص

**Na kama atasoma sura zingine sio vibaya.**

## BAADA YA KUMALIZA TWAWAFU

Ataondoka aelekee upande wa Swafaa ili akafanye Saayi raundi saba, akikaribia Swafaa ataanza kama alivyoanza Mwenyezi Mungu . Alianzia kwa kusema:

﴿ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلۡمَرۡوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِۖ

***( Hakika vilima vya Swafa na Mar-waa ni miongoni mwa alama za Mwenyezi mungu )*** Albaqara: 158

**Kisha atapanda mlima wa Swafaa:**

Atasimama juuyake akielekea Qiblah na amhimidi Mwenyezi Mungu na kupiga takbirah mara tatu na aombe duaa kwa wingi kabisa hali ya kuinua mikono yake, aseme : ***( Lailaha ilal-llahu wahdahu laa sharika lahu, lahul-mulku wa lahul-hamdu wa huwa ala kuli shain qadiir, laa ilaha ila-llahu wahdahu anjaza waadah, wanaswara abdahu wahazamal-ahzaaba wahdahu ).***

**Na aikariri dua hii mara tatu:**

Na aombe baina ya maneno hayo dua yoyote aitakayo ,na kama atatosheka na hiyo dhikri tu pia sio vibaya . Na asinyanyue mikono yake ispokuwa wakati wa kuomba tu.Na wala asiashirie mikono wakati anapopiga takbiira .

Kuashiri mikono ni miongoni mwa makosa yaliyoenea kwa wengi miongoni mwa mahujaji na wanofanya umrah.

**Na aikariri dua hii mara tatu:**

Kuelekea Marwa hali ya kutembea,akiomba dua zitakazomuwia nyepesi ,akijiombea mwenyewe,familia yake, na Waislamu kwa ujumla.Na akifika katika alama ya kijani atakimbia sana. Na hili ni kwa wanaume tu sio wanawake, mpaka afike katika alama ya kijani ya pili, atatembea mwendo wa kawaida mpaka kufika Marwah.

## PINDI MWENYE KUFANYA UMRAH ANAPOUFIKA MARWAH:

- Ataelekea qibla na kusema na kusoma nyiradi alizozisoma alipopanda juu ya Swafaa, lakini bila ya kusoma ayah, ataomba dua aitakayo, kisha atateremka na atatembe mpaka kufika katika alama ya kijani atakimbia mpaka kufika kwenye alama ya kijani ya pili, kisha atakamilisha kwa mwendo wa kawaida mpaka kupanda swafa, na hivyo atakamilisha Saayi yakekwa utaratibu huu,mpaka raundi saba, kwenda kwake kutoka Swafa mpaka Marwa ni raundi na kurudi kwake kutoka Marwa mpaka Swafaa ni raundi nyingine ..
- Na hakuna ubaya akiwa amechoka au kapatwa na tatizo lolote la kiafya anaweza kufanya Saayi akiwa kapanda kijibaiskeli (maalum kwa ajili ya watu wenye matatizo). kipeskili ..



***Inakubalika kwa wanawake ambao wamo katika siku zao au wako katika nifasi :*** Kufanya Saayi tu ,lakini Twawafu hapana, Maana sehemu ya Saayi haizingatiwi kwamba imo nda ya msikiti Mtukufu.



NA MIONGONI MWA MAKOSA YALIYO ENEA

- Ni kitendo cha wanawake kukimbia wakati wa Saayi katika zile alama mbili za kijani .



Baada ya kumaliza sayai mwenye kufanya umrah atanyoa au atapunguza nywele zake ,
lakini kunyoa ni bora zaidi,ispokuwa akiwa Nusuki yake ni Tamatui , na tangu muda wa kufanya kwake umra mpaka kuingia wakati wa Hijja ni mfupi sana , basi vizuri zaidi anatakiwa apunguze ,na aje kunyoa wakati wa Hijjah ,lakini atakapo punguza nywele zake ahakikishe iwe ni kichwa chote . Ama wanawake wao wanapunguza kiasi cha pingiri moja ya kidole.



Na kwa hiyo ndiyo inamalizika Vitendo vya umrah.

Na kisha kinamhalalikia kila kitu kilichokuwa ni haramu kwake kwa sababu ya kuhirimia kwake.

# SAAYI MIZUNGUKO SABA INAANZIA SWAFA NA INAMALIZIKIA MARWA




Kukimbia katika alama za kijani ni kwa wanaume tu



# NAMNA YA KUFANYA HIJJAH

{ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ}

**(Hajja ni miezi maalumu )**



# SIKU YA NANE YA DHUL-HIJJAH :

## (( Hajja ni miezi maalumu ))

### YAWMU TARWIYAH .

Yanaanza matendo ya Hajji siku ya nane ya Dhul-hijja, na inaitwa YAWMU TARWIYAH .

Katika siku hii mwenye kufanya hijji ya Tamatui atahirimia hijji asubui, na atafanya kabla ya kuhirimia kwake Hijjah yale aliyoyafanya kabla ya kuhirimia umrah, ambayo ni kuoga na kujitia manukato na kuswali, kisha kuhirimia akiwa mahali alipofikia au anapoishi.

Ama mwenye kufanya ***Qiraan*** na mwenye kufanya ***Ifraad*** wao itakuwa walikuwa bado wako katika ihram yao.

Mwenye kufanya Tamatu na mwenye kufanya Qiran na mwenye kufanya Ifrad wote wataenda Mina kabla ya adhuhuri, na wataswali dhuhur, Aswir, Maghrib na Isha kila swalah ndani ya wakati wake , bila ya kuzikusanya, lakini wanaziswali kwa kuzipunguza swala zenye rakaa nne wanaziswali kwa rakaa mbili. Na watalala usiku wa kuamkia tarehe tisa Dhul-hijah pale mina, na wataswali Alfajiri hapo mina, Na atakaekuwa alifikia mina kabla ya siku ya tarehe nane basi atahirimia palepale mina asubuhi ya tarehe nane. ..

***Iliyo Sunna kwa Haaji ni kulala Mina Usiku wa kuamkia tarehe tisa.***

Mpaka atakaposwali swala ya Alfajiri siku ya tarehe tisa ,atasubiri mpaka jua likichomoza, kisha ataelekea Arafat kwa utulivu na unyenyekevu hali ya kupiga Talbiya na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa namna mbali mbali za dhikri, na kusoma Qur-ani, na kukithirisha Talbiya na kusema Laailaha ilallah, na Allahu akbar, na Alhamdulillah, na kushukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote.

**Kabla ya dhuhuri**



**Swalah za dhuhuri na aswir na maghrib na isha**



**Kulala mina**

# TISA DHUL-HIJJAH

## Siku ya Arafah

Kusimama arafa ni nguzo katika nguzo za hijji, haiwezi kuswihi Hijja mpaka ipatikane nguzo hii, Mtume -swala na salamu zimwendee- amesema :

**( Hajji ni arafah )**

Imepokelewa na Abudaud na Tirmidhi.

Na siku ya arafah ndio bora Kulikomasiku yote ambayo yamechomozewa na jua.
Katika siku hiyo makundi ya mahujaji yanelekea katika uwanja wa Arafat, waislamu wanasimama siku hiyo Arafat kuanzia adhuhuri mpaka jua kuzama, siku hiyo Mwenyezi Mungu atajifakharisha nao mbele ya Malaika wake.
Imekuja katika swahihi muslim kutoka kwa Mama Aisha – Radhi za Mwenyezi Mungu zimwendee- amesema: Kwamba Mtume -swala na salamu zimwendee- amesema:
( Hakuna siku ambayo Mwenyezi mungu anawaacha huru watu sana na Moto kuliko siku ya arafah, na Mwenyezi Mungu husogea kisha akajifakharisha kwa Malaika kutokana na watu wa Arafa, Anasema kuwauliza Malaika:

**Mnadhani hawa wanataka nini ?**

**Tunaomba Mwenyezi Mungu fadhli zake na ihsani yake.**

Kabla ya dhuhuri



**Swalah za dhuhuri na aswir na maghrib na isha**



# TISA DHUL-HIJJAH

## YAWMU ARAFAH

NI SUNNAH….

Anatakiwa ***Haaji*** afike kabla ya adhuhuri pahala paitwapo Namirah kama ataweza, na jua likipinduka aingie katika mipaka ya bonde la Arafa aswali adhuhuri na al-aswir kwa adhana moja na iqama mbili , na abakie hapo Arafa mpaka jua kuzama.. na kuna alama na mabango mengi yenye kubainisha mipaka ya Arafa..

***Arafayote ni pahali ya kusimama.***

Mwenye kufanya hijji yatakikana afanye bidii siku hiyo tukufu, autumie wakati wake kwa Talbiyah na Dhikri, na kukithirisha kuomba msamaha, na kusema Lailaha ilallah, na kushukuru na kumhimidi Mwenyezi Mungu, na amuelekee Allah kwa khushui na unyenyekevu,na kuijtihadia kujiombea mwenyewe , na ahli wake na watoto wake na ndugu zake Waislamu. Ukiingia wakati wa dhuhuri Imam atawakhutubia watu, khutbah ya kuwakumbusha na mawaidha na maelekezo, kisha atawaswalisha mahujjaji dhuhur na aswir kwa kuzikusanya na kupunguza kwa adhani moja na iqama mbili kama alivyofanya Mtume wa Allah -swala na salamu zimwendee- : Na hakuna kuswli kabla yake wala baina yake, wala baada yake chochote.

Na inampasa mwenye kufanya Hijja katika siku hiyo awe mbali na makosa ambayo yatampotezea ujira wake na thawabu katika siku hii tukufu na katika kisimamo hiki kitukufu.



Arafah



Swalah za dhuhuri na aswir na maghrib na isha



After sunset

Muzdalifah

# MAKOSA YALIYOENEA

Katika Siku ya Arafah ….

Mahujaji wengi wanafanya makosa ambayo yatakikana kutanabahi sana nayo, miongoni mwa makosa hayo ni kama haya yafuatayo....

- Kufikia nje ya mipaka ya Arafah na kukaa mahali hapo walipofikia mpaka kuzama kwa jua, kisha wanaondoka kuelekea Muzdalifa. Mwenye kufanya hiyo ajue hana hijjah.
- Kuondoka Arafah kabla ya kuzama kwa jua, na jammbo hilo halikubaliwi, kwa sababu ni kinyume na alivyofanya Mtume -swala na salamu zimwendee- .
- Kusongamana na kusukumana kwa ajili ya kupanda mlima wa arafah, na kutaka kufika kileleni kwake na kuswali juu yake , na jambo hili ni uzushi ambao hauna asli katika sharia . Ukiongezea na madhara yanayoweza kumpata mtu kiafya au katika mwili.

Na miongoni mwa makosa yaliyoenea kwa mahujaji ni kuuelekea mlima wa Arafat wakati wa kuomba duaa.

**Lakini sunnah ni kuelekea Qiblah wakati wa kuomba duaa.**



# Muzdalifa

## PINDI JUA LINAPO ZAMA SIKU YA ARAFA

Misafarayamahujaji itaondoka kwa baraka za Allah wakielekea upande wa Mash`aril-haraam (Muzdalifa ) ili waswali hapo maghrib na isha kwa kukusanya na kupunguza,kwa adhana moja na iqama mbili mara tu wanapofika hapo.Na walale usiku wao hapo hali ya kutaja Allah na kumshukuru kwa fadhila zake na Ihsani yake kwa kuwajaalia kuhudhuria kisimamo cha Arafa.

Baadhi ya mahujaji pindi wanapofika Muzdalifa hufanya baadhi ya makosa ambayo yatakikana watanabahishe nayo. Ambayo miongoni mwayo ni haya.....

- Kuelekea katika kuokota vijiwe kabla hata ya kuswali maghribi na isha, ammbazo zinaswaliwa kwa kuzikusanya na kwa kupunguza.
- Kuitakidi kwamba vijiwe vya jamarati ni lazima viokotwe muzdalifa.
- - Kuosha vijiwe ya jamarat, na jambo hilo halikupokelewa kwa Mtume -swala na salamu zimwendee-kwa alilifanya .

Na sunnah ni kama tulivyo taja kwamba mtu alale katika usiku huo wa Muzdalifa mpaka wakati wa swala ya alfajiri .
Na wameruhusiwa wanawake na wasiojiweza na watoto na wale wanaowasaidia hawa kuondoka kuelekea mina baada ya kupita nusu ya usiku, baada ya kuzama mwezi .
Pindi akimaliza kuswali ya al-fajri, ni sunnah kwake asimame katika masharil-haraam ( ni mlima katika muzdalifa) , au asimame mahali popote katika muzdalifa, na kuelekea qiblah akithirishe kumtaja Allah na takbir, na duaa kiasi kitakacho muwezekania. Kisha ataondoka kabla ya jua kuchomoza, na huku akiwa anatembea kuelekea mina ataokota vijiwe viya kutupa, ni vijiwe saba ambavyo vinakuwa vikubwa kidogo mfano wa punje ya hummus (kama mfano wa karanga) kwa ajili ya kutupa vijiwe hivyo katika jamaratul-aqaba, ambalo ndilo kuta kubwa, ama vijiwe vingine atavichukua hapo mina.
Na kisha ataendelea na mwendo wake kwa braka za Allah kuelekea mina huku akifanya talbiya kwa khushuui na kukithirisha kumtaja Mwenyezi Mmungu .

Labbaika allahuma labbaika .. labbaika laa sharika laka labbaik…
innal-hamda wan-niimata laka wal-mulk.. laa sharika lak .

Wakati wa kuzama



Kwenda muzdalifa



Swala ya maghrib
Kukusanya na Kupunguza

Kulala muzdalifa

Swala ya alfajiri

Dhikrinadua

Kuokota vijiwe



Kwenda mina

# PINDI HAJI ANAPOFIKA MINA

Aelekeemojakwamojakunako jamratul-aqabah, ambalo Lililokaribu karibu na Makkah , akifika jamratul-aqabah atakata talbiya, kisha atafanya yafuatayo:-

1



Atatupa vijiwe jamratul-aqaba vijiwe saba mfululizo na kupiga takbir kwa kila kijiwe.



2



Atachinja mnyama wake ikiwa anawajibikiwa mnyama ,atakula katiaka mnyama huyo, na atawalisha mafaqiri kama ikimuwia rahisi, na kamahawezi basi amuwakilishe mtu wa kumfanyia hayo.



3



Atanyoa au Atapunguzanywelezake, na kunyowa ndio bora , lakini kwa mwanamke atapunguza kwenye nywele zake kiasi cha ncha ya kidole.



Na mpangilio huu ndio bora katika matendo ya siku hii.
Lakini akitanguliza baadhi au akachelewesha baadhi hakuna makosa.

# SIKU YA KUCHINJA

## SIKU YA KUMI YA DHUL-HIJJAH

**Kwenda iamaratul aqaba**



**Ataacha kupiga takbirah**

**Atatupa jamaratul aqaba**

**Atapiga takbira ya idd**



**Atachinja mnyama**



**Atanyoa au atapunguza nywele**

Waislamu wote duniani mashariki na magharibi pamoja na Mahujaji kwa namna ya peke ,wanaikabili siku ya Eidil-adh-haa yenye kubarikiwa ,wakiwa na furaha na wenye kujibashiria kwa neema za Mwenyezi Mungu alizo waneemesha, na huku wakichinja vichinjwa vyao hali ya kujikurubisha kwa Allah aliye takasika na kutukuka. Na haaji ataanza kupiga takbira za Idi baada ya kupiga Jamaratil-aqabah kwa kusema : Allahu akbar Allahu akbar Allaah Akbar, la›ilaaha ila-llah.. Allaahu akbar Allahu akbar walillahil-hamdu.

Na kuna makosa mengi yanayo fanywa na baadhi ya mahujaji wakati wa kupiga jamarati, miongoni mwayo ni haya:

- Kuitakidi baadhi yao kwamba wanampiga Shaitwaani ,kwa wanatupa mawe kwa hasira pamoja na kusema maneno mabaya, na matusi ati wanamtukana shaitwani . Hakika kimewekwa kitendo cha kutupa mawe lengo lake ni kudumisha utajo wa Allah.
- Kutupa jamarat kwa kutumia mawe makubwa au kwa viatu, au mbao,na mambo yote haya ni katika kuchupa mipaka ndani ya Dini ,jambo ambalo Mtume wetu – Sala na salamu zimwendee- amelikataza
- Kusongamana na kupigana wakati wa jamaraat kwa ajili ya kutupa mawe, na jambo hilo ni kosa kubwa . Kinacho mpasa Haaji ni kuwa mpole kwa ndugu zake Mahujaji, na kujitahidi atupe vijiwe vyake katika sehemu sahihi ndani ya Haudh, haijalishi jiwe limepiga ukuta au halikupiga, muhimu nikwamba liingie ndani ya uzio.
- Kutupa vijiwe viyote mara moja, na katika hali kama hiyo haitahesabiwa ispokuwa kijiwe kimoja tu . Kinachotakiwa ni kutupa kijiwe kimoja kimoja na kupiga takbira kila anapo rusha kijiwe hicho.

Mwenye kufanya Hijah akisha piga jamratul-aqabah na akanyoa au akapunguza nywele,basi hapo anakuwa kapata tahalluli ya kwanza,

yaani mambo aliyokuwa amekatazwa kuyafanya kwa sababu ya Ihraam sasa anaruhusiwa kuyafanya ispokuwa tu hana ruhusa ya kubashiriana na mke wake .

# JAMARAT
# WAKATI WA KUFIKA MINA

1 Asubuhi ya siku ya idi fanya yafuatayo :



Fanya haraka kupiga jamratal-Aqaba tu kwa vijiwe saba, unapiga takbira kwa kila kijiwe kwa kusema : Allahu akbar.




2 Masiku ya tashriq yote:

Piga vijikuta vyote vitatu kidogo cha kati na jamaratal aqabah, kila jamarah vijiwe saba , na kilakijiwe unacho kirusha unapiga takbira .



# TAWAFUL-IFADHAH

## NGUZO KATIKA NGUZO ZA HAJJ

TawafuL-ifadha ni nguzo ambayo kama mtu ataiacha Hijja yake haiwezi kukamilika mpaka aitekeleze nguzo hiyo. Baadaya kutupama we jamratul-aqabah asubuhi yasikuyaiddatakwenda Makkah kwa ajili kutufu ma mara saba ambayo ni Twawaaful-ifaadhwa , na baada ya hapo atafanya Saayi mara sabaendapo nusuki yake ilikuwa ni Tamatui. Au kwa mwenye kufanya nusuki ya Qiraan au Ifraad kama itakuwa alikuwa hajafanya Saayi ya hijah mwanzo pale alipofanya twawaaful-quduumi.



**Inaruhusiwa...**

Kuichelewesha tawaful-ifadhah mpaka baada ya masiku ya Mina, na kwenda Makkah baada ya kumaliza kutupa jamarat..

Baada ya Haaji kumaliza kutupa mawe na kunyoa na tawaful-ifadhah na Saayi kwa mwenye saayi , sasa atahalalikiwa kila kitu kilichokuwa kimekatazwa kwa ajili ya ihraam, mpaka mkewe, atakuwa halali sasa.

# MASIKU YA TASHRIQ

**Yanaanza kwa kuingia usiku wa tarehe kumi na moja ya dhul-hijjah**

- Baada ya tawaful-ifadhah katika siku ya kuchinja atarudi Haaji kuelekea mina ili apate kulala hapo zile siku tatu za Tashriiq.
- Au kwa ajili ya kulala siku mbili kwa yule anaetaka kufanya haraka kufwata Maneno ya Mwenyezi Mungu :

وَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْدُودَٰتٍ ۚ فَمَن تَعَجَّلَ فِى يَوْمَيْنِ فَلَآ إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَن
تَأَخَّرَ فَلَآ إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ لِمَنِ ٱتَّقَىٰ ۗ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٣﴾

Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazohisabiwa. Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili si dhambi juu yake, na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake.

**The 11th of Dhul Hijjah**

**The 12th of Dhul Hijjah**

**The 13th of Dhul Hijjah**

**Na yaliyo wajibu juu ya ya Haaji ...**

- Kupiga Jamaraati tatu katika masiku atakayokuwa mina.
- Kupiga takbir kwa kila kijiwe .
- Kukithirisha dhikri na Duaa
- Kulazimiana na utulivu na utaratibu.
- **Na ajiepushe na kusongamana na kugombana na kubughudhiyan na watu.**



# MWONGOZO WA KUTUPA JAMARAT

- **Ni Sunnah …**

  Kwa Haaji asimame baada ya kupiga kuta la kwanza na la pili hali akielekea Qibla na anyanyue mikono yake aombe chochote akitakacho,bila ya kusababisha msongamano na kusukumana na watu...

**Ama kwenye jamarah kubwa ambalo linaitwa jamratul-aqabah hapo hatasimama wala hataomba dua .**

- Na mwenye kutaka kufanya haraka kuondoka baada ya siku mbili, wajibu kwake ni kupiga jamaraati zote tatu katika siku hiyo ya kumi na mbili, kisha ataondoka kutoka mina kabla ya jua kuzama, ama jua likizama na yeye bado yuko mina basi itamlazimu kubakia mina na kulala hapo usiku wa kumi na tatu na kutupa mawe siku hiyo ya kumi na tatu..

  Endapo atakuwa alikuwa hakujiandaa kuwahi kuondoka. Lakini kama alikuwa kajiandaa kuondoka siku hiyo ya kumi na mbili ,basi haitamlazimu kulala mina .



# TAWAFU YA KUAGA

**Baada kutoka mina**

Ataelekea Haaji katika Mji wa Makka tukufu kwa ajili ya kutufu katika nyumba kongwe, baada ya makundi ya mahujaji kumaliza kutekeleza ibada yao kwa kutimia nguzo zake na wajibu zake ,basi iwe twawafu ya kuaga ndio kitu cha mwisho wanachokifanya katika nyumba tukufu ya Allah… kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mtume – Sala na salamu za Allah zimwendee- ambaye amesema :

***"Mmoja wenu asiondoke mpaka iwe sehemu yake ya mwisho ni katika nyumba ya Allah".***

Imepokewa na Bukhari na Muslim.

Na tawafu ya kuaga ndio jambo la mwisho katika mambo ya wajibu katika ibada ya Hijjah.

Na inamlazimu Haaji aitekeleze kwa muda mchache kabla ya kusafiri kwake kurejea nchini kwake.

Na hakuna mwenye kusamehewa kufanya tawafu ya kuaga ispokua mwanamke ambaye yuko katika siku zake au mwenye nifasi , hawa wanasamehewa twawafu hii, wala hawana fidia yoyote .



# FAIDA

## NGUZO NA WAJIBU ZA HAJJ

| NGUZO ZA HAJJI | 4 |
|---|---|
| 1 | Ihram |
| 2 | Kusimama Arafah |
| 3 | Tawaful-ifadhah |
| 4 | Saayi |

Mwenye kuacha nguzo moja hija yake haija kamilika

**Mwenye kuacha nguzo hijjah haiwezi kutimia.**

| WAJIBU ZA HAJJ | 7 |
|---|---|
| 1 | Kuhirimia katika miqat |
| 2 | Kusimama arafah mpaka kuzama jua |
| 3 | Kulala muzdalifa |
| 4 | Kulala mina usiku wa masiku ya tashriq |
| 5 | Kutupa jamarat |
| 6 | Kunyoa au kupunguza nywele |
| 7 | Tawafu ya kuaga |

Mwenye kuacha wajibu wa hijja atachinja mnyama kama fidia, mbuzi atamchinjia makkah na kugawa nyama kwa mafaqiri wa Makkah, na yeye hata kula katika nyama hiyo.

Mwenye kuacha wajibu badala yake achinje myama.

# HUKMU ZINAZO WAAHUSU WANAWAKE WAUMINI



# HUKMU ZINAZO WAAHUSU WANAWAKE WAUMINI

Masharti yakuwajibikiwa Hijjah kwa wanaume na wanawake

- Uislamu
- Akili
- Kubaleghe
- Uhuru
- Uwezo

**Ama kwa upande wa wanawake wao kuna sharti la kuwa na Mahramu wake.**

Nayeye ndio atasafiri naye katika safari ya Hijjah, kama mume wake au mtu ambaye ni haramu kwake kumuoa uharamu wa milele,kwasababu ya nasabu, kama baba yake mzazi, au mwanae wa kiume ,au kaka yake , au kwa sababu ambayo bi halali kama kaka wa kunyonya naye, au mume wa mama yake, au mtoto wa mume wake.

Na dalili ya hayo ni hadithi ya Ibn Abas - Allah amuwie radhi- yeye amemsikia Mtume – Sala na salamu za Allah zimwendee- akisoma khutuba na akasema : ( Wasikaefaragha mwanaume na mwanamke ispokuwa awepo mahram , na asisafiri mwanamke mpaka awe na mahramu wake, mtu mmoja akasimama na akasema: Ewe Mtume waAllah;Hakika mke wangu ameondoka kuelekea Hijjah ,na mimi nimepangwa kuelekea vitani,Mtume akamwambia: Nenda ukahiji na mkeo» . Imepokewa na Bukhari na Muslim.

Na kutoka Ibn Umar- radhi za Allah ziwe juu yao - amesema Mtume -Sala na salamu za Allah zimwendee amesema:

**( Haikubaliwi mwanamke kusafiri siku tatui spokuwa awe na mahram ).**

Imepokewa na Bukhari na Muslim.

Na hadithi kuhusu jambo hili ni nyingi mno zinazo mzuwia mwanamke kusafiri safari ya Hijja na safari zinginezo bila ya kuwa na mahram wake, kwasababu mwanamke ni dhaifu , yanamtokea mambo mbali mbali na matatizo mbalimbali katika safari yake, mambo ambayo yanawahitajia wanaume kuyatatua ,lakini pia mwanamke anatia tamaa kwa watu ambao ni waovu ,kwa hiyo hapana budi awe na ..mahramu wake atakaye weza kumchunga na mambo kama haya

# MAELEKEZO

**Mahram ambae anasafiri na mwanamke inatakikana awe na masharti yafuatayo:**

Uislamu

Akili

Kubaleghe

Akikata tamaa ya kutompata mahram wa kusafiri naye ,basi inamlazimu amtafute mtu atakaye hijji kwa niaba yake .

MIONGONI MWA HUKMU ZA MWANAWAKE KATIKA IHRAM NI HIZI ZIFATAZO:

1. Ikiwa Hijja ni ya sunnah lazima apate idhini ya mume wake,kwasababu kusafiri kwake kutamkosesha baadhi ya haki zake,na mume ana haki ya kumzuwia kama Hijja itakuwa sio ya faradhi.
2. Inakubalika manamke kumuhijia mwanaume na kumfanyia Umrah kwa makubaliano ya wanazuoni , kama ambavyo pia anaweza kuwa naibu wa mwanamke mwenzie katika kutekeleza ibada hii ,sawasawa awe ni binti yake au mwengine tu.
3. Mwanamke akiwa njiani kuelekea kwenye Ibada ya hijja ,akatokewa na siku zake au Nifasi, ataendelea na safari yake na atakamilisha ibada yake ,na atafanya yote wanayo yafanya wanawake wenzie ambao wako twahara,ispokuwa yeye hatafanya twawafu . Hali hiyo ikimtokea wakati wa kuhirimia atahirimia tu kama kawaaida maana nia haihitajii kuwa twahara.
4. Manamke wakati wa kuhirimi atafanya yote wanayo yafanya wanaume, kama kuoga ,kujisafisha ,na kuondoa uchafu anaotaka kuuondoa kama nywele za chini, kucha . Na sio vibaya kama atajitia manukato mwilini , lakini yasiyotoa harufu sana . Kutokana na hadithi ya Mama A`isha amesema :

«Tulikuwa tunatoka na Mtume – sala na salamu za Allah zimwendee- tunapaka miski katika nyuso zetu wakati wa ihramu ,mpaka mmoja wetu akitokwa na jasho,miski inachuruzika usoni mwake,na Mtume anaiona wala hakutukataza» .

Imepokewa na Abudaud.

# WANAWAKE WAUMINI

5. Wakati wa kutia nia ya ihram mwanamke atavua niqaabu kama atakuwa kaivaa kabla ya kuhirimia . Amesema Mtume -Sala na salamu za Allah zimwendee- :
« Haruhusiwi kuvaa niqaabu mwanamke akiwa katika ihraam». Imepokewa na Bukari.

Na atafunika uso wake kwa kitu kingine ambacho sio niqaabu ,kama kweka juu yake mtandio au nguo ambayo ataitumia kujifunika wakati anapokuwa na wanaume ambao sio mahram kwake , pia atafunika viganja vyake kwao lakini sio kwa kuvaa gloves , maana kauli sahihi nikwamba uso na viganja ni lazima manamke avisitiri katika hali ya kuhirimia na katika hali ya kawaida .

6. Mwanamke anaruhusiwa akiwa kahirimia kuvaa nguo yoyote katika nguo za wanawake ambayo haina mapambo, wala isifanane na mavazi ya kiume ,wala isiwe ya kubana yenye kuonyesha maungo yake ,na isiwe fupi yenye kuonyesha miguu au mikono yake, bali yatakiwa iwe nzito na pana.

Na wamekubaliana wanazuoni kwamba mwanamke katika hali ya kuhirimia anaruhusiwa kuvaa gauni, mtandio, suruwali, khofu, na halazimiki kuvaa nguo ya rangi maalumu, bali anavaa rangi yoyote atakayo miongoni mwa rangi ambazo ni maarufu kuvaliwa na wanawake

7. Ni sunnah kwa mwanamuke aseme talbiyyah baada kuhirimia kiyasi cha kujisikilizisha mwenyewe tu , imekuwa ni karaha kwake kunyanyua sauti kwa kuogopea fitna na ndio maana sio sunna kwa mwanamke kuadhini wala kuqimu, pia ikawa kukumbusha kwake ndani ya swala ni kupiga makofi na sio kusema : Subhaanallah..

( Almughni 2331-330/ )



**Wakati wa kutia nia ya ihram mwanamke atavua niqaabu kama atakuwa**

**Mwanamke anaruhusiwa akiwa kahirimia kuvaa nguo**

**Ni sunnah kwa mwanamuke aseme talbiyyah**

# WANAWAKE WAUMINI

## ANGALIZO

8 . Yampasa mwanamke wakati wa tawaf ajistiri kikamilifu, na sauti iwe ya chini na kuinamisha macho na bila kusongamana na wanaume hasa katika hajarul-aswad au katika Ruknul-yamaaniy ,bali yatakiwa atufu mwisho wa matwaafu , kwasababu kusongamana ni haramu kwa kuchelea fitna , ama kukaribia al-kabah na kubusu Hajarul-aswad ni sunnah ikiwezikana, asifanye haramu kwa ajili ya kutimiza sunnah. Na sunnah kwake ni kuashiria hapo katika Hajarul-aswad pale anapofika usawa wake kwa mbali.



9 . Tawafu ya wanawake na Saayi yao yote inakuwa ni kwenda mwendo wa kawaida . Na wamekubaliana wanazuoni kwamba mwanamke hana wajibu wa kukimbia ,sio katika twawafu wala katika Saayi, na wala hawajibiki kuvaa rubega. Almughni 3/334

Yampasa mwanamke wakati wa tawaf ajistiri kikamilifu

10. Ama ambaye yuko katika siku zake, yeye atafanya matendo yote ya Hijjah ,kuhiriia,kusimama arafa,kulal Muzdalifa,kupiga jamaraati,lakini hatafanya twawafu mpaka atakapo twaharika . Mtume wetu – Sala na salamu za Allah zimwendee- alisema kumwambia mama Aisha kwamba :

Na wamekubaliana wanazuoni kwamba

> « Fanya yote anyoyafanya mwenye kuhiji ,ispokuwa usitufu Alkaaba mpaka utwaharike».

Idhtiba

ANGALIZO..

Akitufu mwanamuke na baada ya kutufu akaingia katika siku zake, basi katika hali kama hii ataruhusiwa kufanya saayi,maana Saayi haishartishwi kuwa na twahara.

Kitabu: Almuminat ya DR. Swaleh alfawzan.

# WANAWAKE WAUMINI

## INAFA



na watu ambaye ni dhaifu kutoka muzdalifa baada ya mwezi kuzama

na kukata nywele cha kichwa chake atakuwa

na atasamihiwa kwake tawafu ya kuwaga

11. Inafa kwa wanawake aende na watu ambaye ni dhaifu kutoka muzdalifa baada ya mwezi kuzama na watatupa jamratul-aqabah wakati ya kufika kwa mina kwa kuogoba kusongamana nawo.
12. Mwanamuke atakata kutoka nywele ya kichwa chake katika hijji na umrah kiyasi ya incha ya kidole na haifai kwake kunyowa.
13. Manamuke ambaye aako na haidhi akitupa jamratul-aqabah na kukata nywele cha kichwa chake atakuwa halali kutoka ihram yake na atakua kwake halali chochote ilikuwa haram kwake kwasababu ya kuhirimia spokua hatakua halali kwa bwana wake paka kutufu tawafal-ifadhah. Akamkubalia nafsi yake kabla ya hiyo fidyah indio atakua wajib juu yake, na hiyo ni kuchinja mbuzi katika Makkah na kubatiya wafaqiri ya haram..
14. Manamuka akikujia haidhi baada ya kutufu tawafal-ifadhah atasafiri baada ya kumaliza hijji yake na atasamihiwa kwake tawafu ya kuwaga kwa hadithi ya Aishah radhi ya Allah zimuendee amesema: Safiyah binti Huyai amekujia haidhi baada ya ifadhah amesema nimeambia hiyo mtume sala na salamu zimuendee amesema: je atatujelewesha??

Nimesema o mtume ya Allah ametufu tawafal-ifadhah kisha alikujia haidhi baada ya ifadhah , Mtume amesema: Sasa aondoke..

Imepokewa na Bukari na Muslim.

Na kutoka Ibn Abas radhi ya Allah zimuendee amesema mtume sala na salam za Allah zimuendee ameamrisha watu awe sehemu yao ya mwisho katika nyumba spokua imesamihewa wanawake wenye haidhi na nifasi.

Imepokewa na Bukari na Muslim.

# MJI WA MADINA NA JINSI YA KUUZURU MSIKITI WA MTUME REHMA NA AMANI ZIMWENDEE



## NAMNA YA KUZURU MSIKITI WA MTUME REHMA NA AMANI ZIMWENDEE

Mji wa Madina ndipo mahala alipohamia Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee, na hapo ndipo alipozikwa.

Katika mji huo upo Msikiti wa Mtume , ambao ni moja kati ya Misikiti mitatu mitukufu ambayo haruhusiwi mtu kuifungia safari ispokuwa miskiti hiyo,kama alivosema Mtume- rehma na amani zimwendee- kwamba: « Haifungwi safari ya kiibada ispokuwa kuielekea miskiti mitatu:

Almasjed Alharam

**Na Msikiti wangu huu (yaani msikiti wa Madina)**

Wal Masjed Alaqsa

Pamoja na kuwa kuuzuru Msikiti wa Mtume sio wajibu wala sharti katika Hijjah,bali pia hakuna mafungamano wala mahusiano yoyote,wala ziara hii haina Ihraamu,ispokuwa ni jambo ambalo linatambulika kisharia,na linapendeza kwa muda wowote ndani ya mwaka.
Kwahiyo pindi Allaha anapomuwafikisha mja,na akamrahisishia kufika katika nchi hii yenye Haramu mbili tukufu basi inakuwa ni Sunna kwake kwenda Madina,ili akaswali katika Msikiti wa Mtume -rehma na amani za Allah zimwensee-,maana kuswali katika msikiti huu swalainakuwa ni bora kuliko kuswali swala elfu moja katika miskiti mingine,ispokuwa Msikiti Mtukufu wa Makkah.



Maana swalakatika Msikiti Mtukufu wa Makkahinakuwa ni sawa na swala laki moja katika miskiti mingine.

# PINDI ANAPOFIKA MWENYE KUFANYA ZIARA KATIKA MSIKITI WA MTUME

Wakati wa kuingia msikitini atatanguliza mguu wa kulia na huku akisema :

**Bismillahi wassalaatu wassalaamu alaa rasuulillah,**

- audhubillaahil-adhwiim,wawajihihil-kariim,wasultwaanihil-qadiim, minashaitwaanir - rajiim.. Allahummaftah lii abuwaaba rahmatika.
- Dua hii pia yatakiwa isomwe wakati wa kuingia katika miskiti mingine.

**Na baada ya kuingia kwakekatika msikiti wa Mtume**

- Ataanza kwa kuswali rakaa mbili za maamkizi ya msikiti,na itapendeza sana kama ataziswali mahala panapoitwa Arraudhwa (ambalo ni eneo lilipo baina ya kaburi ya Mtume na mimbari yake), lakini kama hakuweza basi ataswali sehemu yoyote ile hapo msikitini,kisha ataelekea katika kaburi ya Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- asimame mbele yake hali ya kuielekea, aanze kumsalimia kwa adabu na kwa sauti ya chini, aseme hivi :

(Assalaamu alayka ayyuhan-nabiyyu warahmatullahi wabarakaatuh),
kisha amswalie.
Nakama atasema: Ewe Allah mpe njia na fadhila,na umfufue katika daraja ulilomuahidi,Ewe Allah mpe malipo ya kuutumikia Ummah wake malipo yaliyokuwa bora. Akisema hivyo sio vibaya.

**Kisha anageuka...**

upande wa kulia kidogo ili asimame mbele ya kaburi la Abu-ubakaris-siddiiq- Radhi za Allah zimwendee- atamsalimia na kumuombea rahma na msamaha na radhi.

**Kisha anageuka...**

kidogo tena kuliani kwake,ili asimame mbele ya kaburi la Umar Ibnil-khatwaab -Radhi za Allah zimwendee- atamsalimia na kumuombea rahma na msamaha na radhi.

## Na imegundulika kwamba..

baadhi ya watu wanao uzuru Msikiti wa Mtume- Rehma na amani zimwendee-wanafanya makosa ambayo yanazingatiwa ni miongoni mwa uzushi ambao hauna asili katika Dini,wala haukupokewa kwa Maswahaba .

**Na miongoni mwa makosa hayo ni kama haya yafuatayo....**

- ✗ Kujipangusa katika vyuma vilivyo katika chumba hicho na kuta za msikiti.
- ✗ Kulielekea kaburi wakati wa kuomba dua.
- ✓ Na usahihi ni kuelekea Qibla wakati wa kuomba dua .



## NA NI SUNNA KWAKO EWE MPENDWA MWENYE KUFANYA ZIARA

Kuyazuru makaburi ya watu wa Baqii ambayo wamezikwa Maswahaba wengi sana hapo,ikiwa miongoni mwao ni Khalifa watatu Uthmani -Radhi za Allah zimwendee .

Kuyazuru makaburi ya Mashahidi wa vita vya Uhudi,na miongoni mwaaoni yule bwana wa Mashuhadaa wote ambaye ni Hamza bin Abdil mutwalibi -Radhi za Allah ziwaendee -awasalimie na kuwaombea dua kama ambavyo Mtume – Rehma na amani za Allah zimwendee- alivyowafundisha Maswahaba wakati wa kuzuru makaburi :

« Assalamu alaykum Ahladdiyaar minalmu`uminiina walmuslimina,wainnaa inshaallahu bikum laahiquun,nas-alullaaha lanaa walakumul-aafiyaah».

Aondoke hali akiwa na twahara kwenda katika Msikiti wa Qubaa,ambao ndio Msikiti wa kwanza uliojengwa katika Uislamu,ili akauzuru na apate kuswali humo,kama alivyofanya Mtume mwenyewe na akawahimiza katika hilo ,kama anaviyo sema Sahal bin Saad-Radhi za Allah zimwendee- kwamba Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee amesema:

« من تطهر في بيته ثم أتى مسجد قباء فصلى فيه صلاة كان له كأجر عمرة »

**«Mwenye kujitwaharisha nyumbani kwake,kisha akaelekea katika Msikiti wa Qubaa na akaswali katika Msikiti huo, hupata ujira wa Ibada ya Umrah».**

Pia imekuja katika swahihi mbili (Bukhari na Muslim) katika Hadithi ya Abdallah Bin Umar- Radhi za Allah ziwaendee-amesema: « Mtume -Rehma na amani zimwendee- alikuwa akiuzuru Msikiti wa Qubaa kwa kipandwa au kwa miguu,na anaswali rakaa mbili.

Baada ya Msikiti huu hapo Madina hakuna Miskiti mingine wala maeneo mengine ambayo sharia imetutaka tuyazuru, kwahiyo mtu asijipe tabu na kujipa usumbufu na gharama kwa jambo ambalo halina malipo ndani yake.





# FATWA
# ALLA ANASEMA:

فَسْئَلُوٓاْ أَهْلَ ٱلذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

النحل: ٤٣

**Basi waulizeni wenye kujua ikiwa ninyi hamjui** ". Annahl : 43 "

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

Swali:

Kuna baadhi ya wanao wapa fatwa waliokuja kwa ajili ya Hijjah kwa njia ya anga,kwamba wahirimie wanaposhuka Jiddah,na wengine wanakataa jambo hilo, sasa ni upi usahihi katika swala hili?

Majibu:

Inawalazimu mahujaji wote wanaokuja kwa njia ya anga au ya bahari au nchi kavu wahirimie katika Miiqat ambazo wanazipitia wakija kwa nchi kavu,au kwa usawa wake pale wanapokuwa angani kwenye ndege, au baharini, kwamujibu wa maneno ya Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- alipoziainisha hizi miiqaati kwa kusema :

هن لهن ولمن أتى عليهن من غير أهلهن ممن أراد الحج والعمرة.. "متفق عليه"

Yaani Miiqati hizo ni za watu wa maeneo hayo ,na kila atakaye kuja kupitia maeneo hayo ambaye sio katika watu wa maeneo hayo,kwa watu wanaokusudia kutekeleza Ibada ya Hijjah au Umra.." Hadithi ni Muttafaqun alaihi .
Ama kuhusu Jiddah hiyo sio Miiqat ya wanaokuja kutoka nje ya Jiddah,bali ni Miiqati kwa wakaazi wa hapo hapo Jiddah,na kwa wanaokuja hapo pasina kukusudia Hijjah wala Umra,kisha nia hiyo ikawajia baada ya kukaa kwao hapo Jiddah.
Majibu haya yametolewa na Sheikh Abdul-aziz Bin baazi, Allah amrehemu.

Swali:

Mtu kakusudia kufanya Hijjah yakwake mwenyewe,na alikwisha fanya Hijjah hapo kabla, kisha akiwa Arafa akaamua kubadili nia amuhijie mtu katika ndugu zake,je hukumu yake ikoje? Na je jambo hilo linajuzu au hapana?

Majibu:

Mtu pindi anapohirimia kufanya Hijjah yakwake mwenyewe hana ruhusa baade kubadilisha nia, sio njiani wala Arafa au sehemu yoyote ile,bali inamlazimu ajihijie mwenyewe,wala asigeuze kumhijia si baba yake au mama yake au mtu mwingine, Hijjah itabaki ni yake tu, kwa mujibu wa kauli ya Alla aliposema:

وَأَتِمُّوا۟ ٱلْحَجَّ وَٱلْعُمْرَةَ لِلَّهِ

سورة البقرة الآية ١٩٦

Yaani : « ***Timizeni Ibada ya Hijjah na Umra kwa ajili ya Allah***»
Kwahiyo anapohirimia kwa ajili yake,basi anawajibikiwa kuitimiza,na akihirimia kuhijia mtu mwingine lazima aitimize kwa mujibu wa alivyo hirimia,wala asibadilishe baada ya kuhirimia. Pindi atakapokuwa yeye mwenyewe aliwahi kutekeleza Hijjah.
Majibu yametolewa na Sheikh Abdul-aziz Bin Baazi,Allah amarehemu.

Swali:

Mama yangu alifariki nikiwa mdogo,na alipewa pesa mtu ambaye tunamuamini ili amfanyie mama yangu Hijjah, na pia baba yangu alifariki na mimi sina ninayemjua kati ya wazazi wangu,na nimepata kuskia kwa mmoja kati ya ndugu zangu kwamba baba aliwahi kufanya Hijjah. Je inajuzu kumlipa mtu akamhijie mama yangu?au inanilazimu nikawahijie mwenyewe,na je baba nimuhijie nae ingawanimeskia kwamba aliwahi kuhiji?

Majibu:

kama utawahijia mwenyewe na ukajitahidi kuikamilisha Hijjah yako kwa mujibu wa sharia hiyo ni bora zaidi,na ukimlipa mtu akawahijie ,ambaye ni muaminifu na mwnye Dini,sio vibaya. Lakini bora zaidi uwatekelezee Hijjah na Umra,hivohivo utakaye mlipa kwa kazi hiyo unatakiwa kumuamuru awatekelezee Hijjah na Umra, na jambo hilo ni miongoni mwa mema yako kwa wazazi wako. Allah akutakabalie wewe na sisi pia. Majibu haya yametolewa na Shekh Abdul-azizi Bin Bazi , Allah amrehemu.

Swali:

Mwanamke katekeleza Ibada ya Hijjah, na akafata utaratibu wake wote ispokuwa hakupiga Jamaraati(hakutupa mawe), alimpa mtu jukumu la kumpigia kwa niaba,maana yeye alikuwa na mtoto mchanga, na Hijjah hii kwake ni Hijjah ya faradhi. Ni ipi hukumu ya tendo lake hili?

Majibu:

Hana kosa lolote hapo,maana kitendo cha kumpigia mtu kwa niaba kinatosheleza,kutokana na hatari ya msongamano unaokuwepo wakati wa kutupa mawe hasa kwa upande wa wanawake na wenye watoto.

Majibu yametolewa na Shekh Abdul-aziz Bin Bazi Allah amrehemu.

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

Swali:

Je inafaa mtu kumuusia mtu mwengine amfanyie Hijjah na ilihali yeye bado yu hai ?

Majibu:

Ikiwa huyu anayeusia au anayetaka afanyiwe Hijjah yeye hawezi kwa sababu ya utu uzima au maradhi ambayo hayatarajiwi kupona,basi hakuna ubaya kufanya hivyo,kutokana na mapokezi yaliyothibiti kwamba Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- alimwambia mtu mmoja alie mshitakia kwamba mzazi wakehawezi kuhiji wala hawezi kusafiri,alimwambia :

"حج عن أبيك واعتمر"

Yaani « ***Mhijie baba yako na umfanyie Umra*».**

Na maneno kama haya alimwambia mama mmoja katika kabila la Khath`amah,pale alipomuuliza kwa kusema : Ewe Mtume wa Allah, hakika baba yangu imemdiriki faradhi ya Allah katika wakati ambao yeye hawei kuhiji. Mtume akamwambia:

"حجي عن أبيك"

**« *Mfanyie Hijjah mzazi wako*» .**

Majibu haya yametolewa na Shekh Abdul-aziz Bin Bazi, Allah amrehemu.

Swali:

Kama mtu atakufa na akawa hakumuusia yoyote kumfanyia Hijjah,halafu mwanae akaamu kumuhijia je deni hilo la hija kwake linakwisha ?

Majibu:

Atakapo muhijia mwanae ambaye ni mwislamu na ikawa tayari yeye alikwisha hiji,kwa kufanya hivyo kweli deni kwake litakwisha, ni hivyohivyo hata akimuhijia mtu mwingine ambaye si mwanae, lakini ikawa yeye alikwisha hiji inakubalika, kutokana na hadithi iliypo katika swahihi mbili ( Bukhari na Musli) ,hadithi iliyopokewa na Ibnu Abasi – Radhi za Allah ziwaendee -kwamba mwanamke mmoja alisema kumuuliza Mtume « Ewe Mtume wa Allah,hakika faradhi ya Allah kwa waja wake imemdiriki baba yangu akiwa ni mzee sana,hawezi kuhiji wala kusafiri, je nikamuhijie? Mtume -Rehma na amani zimwendee- akasema

"نعم حجي عنه"

**«*Ndio kamuhijie baba yako*».**

Majibu yametolewa na Shekh Abdul-aziiz Bin Baazi, Allah amrehemu.

Swali:

Swali : Je inajuzu kwa Haaji kuitanguliza Saayi ya Hijjah kabla ya kufanya twaaful-ifaadhwa?

Majibu:

Ikiwa nusuki anayoifanya ni **Ifraad** au ni **Qiraani** huyu inajuzu kwake kuitanguliza Saayi kabla ya twawaaful-ifaadhwa, anaitanguliza pale anapotufu twawaaful-quduum kama alivyofanya Mtume pamoja na Maswahaba ambao walikuwa wamekuja na vichinjwa.

Ama ikiwa nusuki yake ni **Tamatui** huyu anawajibikiwa Saayi mbili..yakwanza ni pale anapofika Makka, ambayo ni ya Umra, ya pili ni ya Hijjah, na hii vizuri zaidi inatakiwa iwe baada ya Twawaaful-ifaadhwa,maana Saayi inafuatana na Twawaafu. Lakini akiitanguliza hakuna ubaya,maana Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- aliulizwa na muulizaji akasema: Nimefanya Saayi kabla sijatufu??naye akamwambia :

"لا حرج"

Yaani : ***Hakuna ubaya*** . Maana Haaji siku ya Idi anafanya mambo matano yanayo fungamana na ibada yake,kwa mpangilio huu:

1- Anatupa mawe (Jamaraati) lile kuta la mwisho tu.
2- Anachinja mnyama wake
3- Ananyoa au kupunguza nywele zake
4- Anafanya twawafu katika nyumba kongwe Alkaaba.
5- Anafanya Saayi kati ya Swafa na Marwaa.

Ispokuwa kama kafanya nusuki ya Qiraani au Ifraad na ikawa alifanya saayi baada ya ile twawaful-quduum. Lakini bora zaidi ni kufuata mpangilio tulio utaja hapo juu, lakini akitanguliza ,hasa kukiwa na sabau inayompelekea kufanya hivyo hakuna uabaya,na hii ni katika Rehma ya Allah na wepesi kwa waja wake.

Majibu yametolewa na Sheikh Muhammad Bin Uthaimin Allah amrehemu.

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

Swali:

Ni ipi hukmu ya mtu aliefanya Umra kwa ajili mzazi wake baada ya kufanya umra yake, kisha akarudia kumfanyia umra mzazi wake kwa kuweka nia kutokea Tan-iim (ambapo ndipo watu wa Makka wanhirimia kwa ajili ya Umrah) , je Umra yake hiyo ni sahihi au inamlazimu akahirimie kwenye Miiqati ya asili (yaani inayo muhusu yeye ) ?

Majibu:

Pindi utakapofanya Umra kwa ajili yako kisha ukamaliza na ukawa huru,na ukataka kumfanyia Umra baba yako ikiwa amekwish akufa au hajiwezi tena,basi unalazimika kutoka nje ya Mipaka ya haram kama vile Tan-iim, na huko unahirimia Umra, wala hulazimiki kusafiri kufuata Miiqati uliyopitia wakati wa kuingia Makkah.
Majibu yametolewa na kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya fat-wah.

Swali:

Je yafaa kuitamka nia wakti wa Kuhirimia ?

Majibu:

Sio katika sharia mwislamu kutamka nia ispokuwa katika ihraam tu,maana hivyo ndivyo ivyopokelewa kwa Mtume -Rehma na amani zimwendee- , ama katika swala na twawaafu,hatakiwi kabisa kuitamka nia akasema kwa mfano: Nanuwia kuswali kadha wakadhaa...au nanuwia kutufu kadha wakadhaa,jambo hilo ni katika Bid`aa,na kuitamka nia ni makosa na kama jambo hilo lingekuwepo kisharia basi Mtume -Rehma na amani zimwendee- angelibainisha na kuliweka wazi kwa Umati wake kwa maneno na vitendo,na wangetutangulia kulifanya wema waliotanguliza miongoni mwa Maswahaba na wengineo. Kwakuwa halikunukuliwa hilo kutoka kwa Mtume -rehma na amani zimwendee-wala halikunukuliwa kwa Maswahaba- Radhi za Alla ziwe juu yao, inatambulika wazi kwamba huo ni uzushi,na Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- amesema: "وشر الأمور محدثاتها" أخرجه مسلم

Yaani : ***" Na shari ya mambo ni yale yenye kuzushwa "***

Imepokewa na Imamu Muslim

Na amesema tena : "من أحدث في أمرنا هذا ما ليس منه فهو رد" متفق عليه .

Yaani : ***" Mwenye kuzua chochote katika jambo letu hili (yaani katika dini), basi hilo atarejeshewa mwenye "*** ni Muttfaqun alaihi

Na katika Tamko la mapokezi ya Imamu Muslim kwamba Mtume -Rehma na amani zimwendee- alisema :

***"Mwenye kutenda aamali yoyote isiyokuwa na amri yetu,basi amali hiyo atarejeshewa mwenyewe ".***

Majibu yametolewa na Sheikh Abdul-aziz Ibnu Bazi ,Allah amrehemu.

**Swali:** Je inajuzu kuchanganya Twawaaful-ifaadhwa na twawaaful-wadai pamoja, ikiwa mwenye kutufu anakusudia kuondoka na kurudi nchini kwake?

**Majibu:** Hakuna ubaya katika hilo, kama mtu atacheleweshа Twawaful-ifaadhwa mpaka atakapokusudia kusafiri na akawa amekamilisha kupiga Jamarati na amemaliza kila kitu,basi Twawaful-ifaadhwa inaitosheleza Twawaaful-wadai. Na kama ataamua kuzifanya zote (yaani Twawaful- ifaadhwa na Twawaaful-wdai) hiyo inakuwa ni kheri juu ya kheri,lakini akitosheka na moja wapo na akanuwia twawaful-wadai,au kwa twawafu yake moja akanuwia mbili jambo hilo linajuzu.

Majibu yametolewa na Shekh Abdul-aziz Ibnu Baz. Allah amrehemu.

**Swali:** Mimi ni miongoni mwa wakaazi wa Mji wa Jidda,nimewahi kufanya Hijjah mara saba,lakini mara zote sikuwahi kutufu twawaful-wadai,kwasababu baadhi ya watu walinambia kwamba watu wa Jiddah hawawajibikiwi twawaaful-ifaadhwa, je Hijjah zangu ni sawa?

**Majibu:** Wakazi wa Jiddah na mfano wao kama watu wa Twaaifu na wengineo hawatakiwi kuondoka Makkah ila baada ya kufanya Twawaaful-wadai,kwa mujibu wa maneno ya Mtume- Rehma na amani zimwendee – aliposema kuwaambia mahujaji:

" لا ينفرن أحد منكم حتى يكون آخر عهده بالبيت "

Yaani : ***" Asiondoke yoyote miongoni mwenu mpaka iwe sehemu yake ya mwisho ni katika nyumba tukufu(Alkaabah) ".***

Na imekuja katika swahihi mbili (Bukhari na Muslim) katika hadithi ya Ibni Abasi -Radhi za Allah ziwaendee- amesema : Wameamrishwa watu iwe sehemu yao ya mwisho ni katika nyumba tukufu (Alkaabah),ispokuwa amefanyiwa wepesi mwanamke ambaye yuko katika siku zake, namwenye kuiacha twawaful-wadai anawajibikiwa kuchinja mnyama, ambaye ni mbuzi au kondoo,au kwa ng`ombe na ngamia mmoja anawatosheleza watu saba, anachinjwa Makkah na kugawiwa kwa mafakiri wa Haram, pamoja na kulazimika atubie na kuomba msamaha kwa Allah,na aweke azma ya kweli kwamba hatarudia tena kufanya kosa hilo.

Majibu yametolewa na Sheikh Abdul-azizi Ibnu bazi . Allah amrehemu.

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

**Swali:**

Mtu alikuwa katika twawafu,alipofika raundi ya tano kwa mfano kabla hajaikamilishaikaqimiwa swala,akaswali kisha akasimama kukamilisha twawafu,je hii raundi ya tano aliyoikatiza kwa ajili ya swala inaingia katika hesabu na anaendelea pale aliposimamia au ataifuta na kuianza tena kuanzia pale Hajarul-aswad ?

**Majibu:**

kiusahihi nikwamba katika hali kama hii raundi yake haiwezi kufutwa,bali ataanzia pale alipoikatishia kwa ajili ya swala.

Majibu yametolewa na Kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya Fatwaa.

**Swali:**

Sisi tunaishi Australia, na kunakundi kubwa la Waislamu wa nchi hii linataka kutekeleza Faradhi ya Hijjah, nasisi safari yetu inaanzia SIDNI kwa mfano, na kituo chetu cha kwanza kitakuwa moja kati ya vituo hivi vitatu vya anga, JIDDAH,ABUDHABI,BAHRAIN, sasa miiqati yetu ya kuhirimia itakuwa wapi? Je tuhirimie pale SIDNI au katika sehemu nyingine?

**Majibu:**

Hiyo SIDNI na ABUDHABI na BAHRAIN siyo Miiqati ya Hijah wala Umra, pia JIDDAH sio Miiqati kwa watu kama ninyi,bali ni Miiqati kwa watuu wanao ishi hapo tu,ninyi kama mtakuja kwa njia ya angani mnawajibikiwa kuhirimia katika Miiqati ya kwanza kabisa mnayo ipitia mkiwa mnakusudia Makkah, kwa mujibu wa maneno ya Mtume – Rehma na amani zimwendee – pindi alipoziainisha Miiqaat:

" هن لهن ولمن أتى عليهن من غير أهلهن ممن أراد الحج والعمرة " .

***" Miiqati hizo ni za watu wa maeneo hayo ,na kila atakae kuja kupitia katika maeneo hayo akikusudia Hijja au Umrah".***
Pia mnaweza kuwauliza watumishi kwenye ndege kabla hamjazivukaMiiqati hizo, pia kama mtanuwia kuingia katika Ihraam ya Hijjah au Umra kabla ya Miiqaati mtakayo ipitia, kwa kuchelea msije mkaivuka bila ya kuhirimia hakuna ubaya kufanya hivyo. Ama maandalizi kwa ajili ya Ihram kwa kufanya usafi au kuoga,na kuvaa mavazi ya Ihraam hii inaruhusiwa mahala popote.

Majibu yametolewa na Kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya Fatwaa.

Swali:

Ni ipi hukmu ya mtu alie hiji akafanya nusuki ya Qiraan lakini hakuchinja wala hakulisha maskini,wala hakufunga,na tayari kishaondoka katika Mji wa Makkah na muda wa Hijjah umemalizika na tayari yuko mbali na nyumba tukufu ya Allah na maeneo ya Ibada ya Hijjah ?

Majibu:

Anawajibikiwa kuchinja mnyama mwenye sifa zinazo zingatiwa katika Udh-hiuakwasababu kafanya Nusuki ya Qiraan,mnayama huyo amchinje mwenyewe au amuwakilishe mtu muaminifu aliyopo Makkah,nyama igawiwe kwa mafakiri wa Haram, na anaruhusiwa kula katika nyama ile na kuwagawia awatakao,na kama hana uwezo wa kichinjwa basi atafunga siku kumi.

Majibu yametolewa na Kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya Fatwaa.

Swali:

Pindi haaji akikamilisha nguzo na waajibu zote za Hijjah ispokuwa Twawaaful-ifaadhwa na wadaai,je itakapokuwa twawaaful-ifaadhwa ni katika siku ya mwisho katika masiku ya Hijjh,ametufu twawaaful-iafaadhwa na hakutufu twawaaful-wadai,aksema inatosha,nayeye sio katika watu wa Makka anatoka katika miji mingine ya Mamlaka, huyu hukmu yake ikoje ?

Majibu:

Ikiwa hali ndio kama ilivyoelezwa, na ikawa kuondoka kwake kulikuwa ni mara tu baada ya kufanya twawaaful-ifaadhwa,basi hiyo itamtosheleza kwa zote mbili endapo atakuwa kamaliza kupiga jamarati..

Majibu yametolewa na Kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya Fatwaa.

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

Swali:

Mimi nimehiji nusuki ya Ifraad,nikafanya twawafu na saayi kabla ya siku ya Arafa, je inanilazimu tena Twawafu na saayi wakati wa kutoka Mina?

Majibu:

Huyu ambaye kafanya Nusuki ya Ifradi na pia kama atafanya Tamatu kisha akaja Makkah na akatufu na akafanya Saayi, na akabakia ktika ihraamu yake akawa hakuzivua, basi huyo ile Saayi aliofanya inamtosha, hivyo atakapotufu siku ya Eid au baada ya siku ya Eid basi hiyo Twawaaful-ifaadhwa inatosha,endapo atakuwa kabakia katika ihraamu yake mpaka siku ya tarehe kumi,au kama alikuwa na kichinjwa maana hana ruhusa ya kutahalal mpaka siku ya tarehe kumi. Na ile saayi aliyoifanya awali imemtosheleza. Ama kwa aliyefanya Nusuki ya tamatui huyo inamlazimu Saayi ya pili mbali naile ya kwanza ambayo ilikuwa ya Umra.

Majibu yametolewa na Kitengo cha kudumu cha utafiti wa kielimu na mambo ya Fatwaa.

Swali:

Ni ipi hukmu ya mtu alie enda Makkah wala hakukusudia Hijjah wala Umra ?

Majibu:

Mtu anayekuja Makkah na akawa hajakusudia Hijjah au Umra kama vile wafanya biashara,na wafanya kazi,na madreva na wengineo ambao wanaingia kwa ajili ya kazi,wao hawalazimiki kuhirimia labda kama watataka wao,kwa mujibu wa kauli ya Mtume-Rehma na amani zimwendee- pindi alipotaja Miiqat alisema :

" هن لهن ولمن أتى عليهن من غير أهلهن ممن أراد الحج والعرة " .

Yaani: ***" Miiqat hizi ni za watu wa maeneo haya na kila atakyekuja Makkah kupitia katika maeneo hayo, ambaye sio mkaazi wa hapo, na ikawa kuingia kwake Makkah anakusudia Hijja na Umra ".***

Kwahiyo imefahamika kwamba atakayepita katikaMiiqat ilihali hakusudii Hijjah wala Umra halazimi kuhirimia, nahii ni katikarehma za Allah kwa waja wake na kuwafanyia wepesi.

Rejea kitabu: Attahqiiq wal-iidhwaah -cha Sheikh Abdul-aziiz Ibnu Baaz.

**Swali:** Mwenye kufanya Nusuki ya Tamatui na mwenye kufanya Qiraani pindi wakishindwa kuchinja watafanya nini ?

**Majibu:** Atakaposhindwa kuchinja alie hirimia Tamatui au Qiraani ataazimika kufunga siku tatu ndani ya masiku ya Hijjah na siku saba baada ya kurejea kwake. Na anakhiyarishwa katika kufunga masiku haya matatu,akipenda anafunga kabla ya tarehe kumi (Yaumun-nahri), na akipenda atafunga ndani ya zile siku tatu za tashriiq (yaani tarehe kumi na moja mpaka tarehe kumi na tatu za mwezi wa Dhul-hijjah) . Allah amesema:

وَأَتِمُّوا۟ ٱلْحَجَّ وَٱلْعُمْرَةَ لِلَّهِ ۚ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا ٱسْتَيْسَرَ مِنَ ٱلْهَدْىِ ۖ وَلَا تَحْلِقُوا۟ رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ ٱلْهَدْىُ مَحِلَّهُۥ ۚ
فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ بِهِۦٓ أَذًى مِّن رَّأْسِهِۦ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ۚ فَإِذَآ أَمِنتُمْ فَمَن تَمَتَّعَ
بِٱلْعُمْرَةِ إِلَى ٱلْحَجِّ فَمَا ٱسْتَيْسَرَ مِنَ ٱلْهَدْىِ ۚ فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٍ فِى ٱلْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ ۗ تِلْكَ عَشَرَةٌ
كَامِلَةٌ ۗ ذَٰلِكَ لِمَن لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُۥ حَاضِرِى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾

Yaani : ***" Timizeni Hijjah na Umra kwa ajili ya Mwenyezi mungu, na ikiwa mkizuiwa ,basi ( chinjeni ) wanyama walio wepesi kupatikana . Wala msinyowe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjoni mwao. Na atakayekuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidia kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama . Na mtakapokuwa salama , basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kasha ndio akahiji, basi achinje mnyama alie mwepesi kumpata. Na asiyepta, afunge siku tatu katika hijjah na siku saba mtakaporudi ,hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu . Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu"*** . Albaqara : 196

Na imekuja katika Swahihil-Bukhari katika hadithi ya Mama A`aisha na Ibnu Umar -Radhi za Allah ziwaendee- wamesema :

> **" Haikutolewa ruhusa ya kufunga katikamasiku ya Tashriiq ispokuwa kwa yule ambaye hakupata kichinjwa "**

Na bora zaidi kama atatanguliza kuzifunga siku hizi tatu kabla ya siku ya arafa,ili siku ya Arafa asiwe kafunga, maana Mtume -Rehma na amani zimwendee- alismam Arafa akiwa hajafunga,na akazuwia kufunga kwa wale waliosimama Arafa. Na masikuhayo kuna ruhusa kuyafunga mfululizo au kwa kuyaachanisha,kadhalika zile siku saba sio lazima kuzifuatanisha,maana Allah hakushartisha kuzifuatanisha pale aliposema :

"***" ... Na masiku saba pindi mtakapo rejea".*** وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ

Na kufunga kwa asiyekuwa na uwezo wa kichinjwa ni bora kuliko kiombaomba ili apate kichinjwa.

Rejea kitabu: Attahqiiq wal-iidhwaah -cha Sheikh Abdul-aziiz Ibnu Baaz.

# FATWA

**Swali:** Ni ipi hukmu ya mtu aliefika katika Miiqat katika miezi ambayo sio miezi ya Hijjah?

**Majibu:** Mwenye kufika katika Miiqat anahali mbili:

***Kwanza :*** Anaweza kufika katika miezi ambayo sio miezi ya Hijjah, kama mwezi wa Ramadhani au Shaabani. Kwa mtu huyu ni Sunna kwake ahirimie Umrah kwa kusema : ***LABBAIKA ALLAAHUMMA UMRATAN,*** akithirishe talbiya mpaka atakapofika Alkaaba, hapo atakata talbiya,atafanya twawafumara saba,ataswali rakaa mbili nyuma ya Maqaamu Ibraahim,kisha ataelekea Swafaa atafanya Saayi mara saba baina ya swafa na Marwaa, kisha atanyoa au kupunguza nywele zake. Kwa kufanya hivyo atakuwa kamaliza Umra yake na atahalalikiwa kila kitu kilichokuwa kimezuiliwa kwake kwa sababu ya ihraam.

***Pili :*** Anaweza kufika katika Miiqaat ndani ya miezi ya Hijjah ambayo ni Shawaali , Dhul-qaadah na Masiku kumi ya mwanzo ya mwezi wa Dhul-hijjah..

Mtu kama huyu anakhiyaarishw baina ya mambo matatu, imma afanye Hijja pekeyake, imma afanye Umra pekeyake, imma achangaye Hijja na Umra. Maana Mtume – Rehma na amani zimwendee- alipofika katika Miiqat katika mwezi wa Dhil-qaada katika Hijja yake ya kuaga,aliwakhiyaarisha Maswahaba wake baina ya hizi Nusuki tatu. Lakini ni sunna kwa huyu kama atakuwa hakuja na kichinjwa,ahirimie Umrah na afanye yale tuliyoyataja hapo nyuma kuhusu Umra, kwasababu Mtume – Rehma na amani zimwendee- aliwaamuru Maswahaba wake walipokaribia kuingia Makkah wafanye Ihraamu zao iwe ni Umra na akawasistiza hilo.

Rejea kitabu: Attahqiiq wal-iidhwaah -cha Sheikh Abdul-aziiz Ibnu Baaz.

**Swali:** Mama yangu ni mtu mzima sana na anataka kufanya Hijjah , lakini hana mahramu mahramu na kumpata Mahram kutamkalifu pesa nyingi, katika hali kama hii ni ipi hukmu yake ?

**Majibu:** Huyo hawajibikiwi Hijjah,maana mwanamke haruhusiwi kuhiji bila ya kuwa na Mahram sawasawa aweni binti aumtu mzima. Ikimuwia vyepesi kupata mahram basi atahiji, na endapo atafariki kabla ya kuhiji basi litatolewa fungu katika mali yake akafanyiwe hijjah, na kama mtu akimfanyia Hijjah kwa mali yake mwenyewe bila kuhitaji kupewa chochote ni vizuri zaidi.

Majibu yametolewa na Sheikh Abdul-aziz Ibnu Baz. Alla amrehemu.

**Swali:** Ni wakati gani inafaa kumuwakilisha mtu akakupigie jamarati? Na je kuna masiku ambayo haijuzu kumuwakilisha mtu katika kupiga jamarati ?

**Majibu:** Inajuzu kumuwakilisha mtu katika kupiga jamarati zote endapo mtu atakuwa ni mgonjwa hawezi kutupa mwenyewe ,au mja mzito anaogoapa msongamano wa watu, au anaye nyonyesha lakini hana mtu wa kumuachia mtoto,kadhalika mzee kikongwe na mfano wa watu kama hawa ambao hawawezi kupiga jamaraati wenyewe, hivyohivyo mawalii wanao hiji na watoto wao wanatakiwa kuwapigia mawe kule jamaraati. Kwahiyo mtu huyu ambaye anamtupia mtu inatakiwa atupe ya kwake kwanza kisha amtupie mtu ambaye kamuwakilisha kumtupia, lakini ifahamike kuwa haijuzu kumtuma mtu ambaye hayuko katika ibada ya Hijjah.

Majibu yametolewa na Sheikh Abdul-aziz Ibnu Baz. Alla amrehemu.

# FATWA
# ALLA ANASEMA:

**Swali:** Je inajuzu kwa mwanamke kutumia vidonge vya kuzuwia siku zake au kuzichelewesha ndani ya masiku ya Hijjah?

**Majibu:** Naam inajuzu kwa mwanamke kutumia vidonge vya kuzuwia siku zake wakati wa Hijjah kwa kuchelea ada yake isije kumuharibia kukamilisha ibada yake, lakini jambo hilo liwe baada ya kupata ushauri wa Daktari kwa ajili ya usalama wake, kadhalika katika mwezi wa Ramadhani akipenda ashirikiane na watu wengine katika funga.

**Swali:** Mimi nimevaa Niqaabu wakati wa kufanya Umra bila ya kujua kwamba hairuhusiwi, je kafara yake ni ipi ?

**Majibu:** Kwakuwa Niqaabu ni miongoni mwa vitu vilivyo zuiliwa wakati wa ihraam ,basi kinachomuwajibikia ni kutoa fidia,ambayo ni kichinjwa,au awalishe maskini sita,au afunge siku tatu ,lakini kwasharti awe alifanya hivyo akiwa anajua, na alikumbushwa. Maana akiivaa mtu bila kujua hukmu au kwa kusahau kwamba yuko katika ihraam, basi hawajibikiwi fidia .

Majibu yametolwa na Sheikh Abdul-aziz Bin Abdallah Ibnu Baaz, Allah amrehemu.

# DUA

## Alla amesema:



وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡ

**"NA AMESEMA MOLA WENU NIOMBENI NITAKUJIBUNI"**

# DUA SIKU YA ARAFA

Imepokewa kwamba Mtume – Sala na salamu zimwendee- amesema : « Bora yaDua ni Dua inayoombwa siku ya Arafa, na bora dua niliyoomba mimi na Manabii kabla yangu ni : ***LAAILAAHA ILLA LLAAHU WAHDAHU LAA SHARIIKA LAHU LAHUL-MULKU WALAHUL-HAMDU YUHYII WAYUMIITU WAHUWA ALAAKUL-LI SHAI` IN QADIIR.***

Na pia imeswihi kutoka kwa Mtume – Sala na salamu zimwendee- kwamba amesema : « Maneno yanayopendwa na Allah ni manne: ***SUBHAANALLAHI WAL-HAMDULILLAAHI, WALAAILAAHA IL-LALLAHU ,WALLAAHU AKBAR*»*.**

Kwahiyo inatakikana kukithirisha Dhikri hii, kuirudiarudia kwa utulivu na unyenyekevu, na inatakikana pia kukithirisha Dhikri na Dua zilizopokelewa kisharia kila wakati, hasahasa katika maeneo haya na katika siku hii tukufu, na mtu achague Dhikri na Dua ambayo inajumuisha mambo mengi, miongoni mwa Dua na Dhikri hizo ni kama hizi zifuatazo:

- SUBHAANALLAAHI WABIHAMDIHI, SUBHAANALLAAHIL-ADHWIIM.
- LAAILAAHA ILLAA ANTA SUBHAANAKA IN-NII KUNTU MINADHWAALIMIIN. LAAILAAHA ILLA LLAAHU WALAA NAABUDU ILLAA IYYAAHU ,LAHUN-NIIMATU WALAHUL-FADHLU, WALAHU THANAAUL-HASAN.
- LAAILAAHA ILLALLAAHU MUKHLISWIINA LAHUD-DIIN WALAU KARIHAL-KAAFIRUUN.
- LAAHAULA WALAA QUWWATA ILLAA BILLAAAHI.
- RABBANAA AATINAA FID-DUNIYAA HASANATAN ,WAFIL - AAKHIRATI HASANATAN, WAQINAA ADHABAN-NAAR.

Alla amesema :

وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

«Na amesema Mola wenu niombeni nitakujibuni,hakika wafanyao kibri katika kuniabudu , wataingia katika jahannam wakiwa wamedhalilika».

Na amesema Mtume – sala na salamu zimwendee- kwamba : ***« Hakika Mola wenu ni mwenye haya na ni mkarimu,humuonea haya mja wake pindi anaponyanyua mikono kwake kuirejesha mitupu».***

Na amesema pia Mtume – Sala na salamu zimwendee- kwamba : « Hakuna mwislamu yoyote anayemuomba Allah maombi ambayo hayana madhambi ndani yake wala kukata udugu,ispokuwa humpa kwa maombi yake hayo moja ya mambo matatu, ima atapewa kwa haraka alichokiomba,, ima atawekewa iwe ni akiba yake ya akhera,na ima ataondoshewa jambo baya kulingana na maombi yake» . Maswahaba wakasema : Kwahiyo tukithirishe maombi? Mtume – Sala na salamu zimwendee- akasema : « ... Alla ni mwenye kukithirisha zaidi» .

# MIONGONI MWA ADABU ZA MAOMMBI

**Kuwa na Ikhlaasi katika kuomba**

- Aanze kwa kumhimidi Allah na kumsifu na kumswali Mtume, kisha aombe na ahitimishe maombi yake kama alivyoanza kwa kumhimidi Allah na kusifu na kumswali Mtume.
- Awe na azma katika maombi yake na awe na yaqini ya kujibiwa .
- Awe ni mwenye kurudiarudia (aombe sana) na asiwe na haraka katika maombi yake.
- Moyo wake uwe haadhir wakati wa maombi
- Awe mwenye kuomba wakati wa raha na wakati wa shida.
- Asimuombe ispokuwa Allah pekeyake.
- Asimuombee dua mbaya mke wake au mali yake au watoto wake au yeye mwenyewe kujiombea dua mbaya.
- Ainamishe sauti yake,maombi yake yawe kwa sauti ya kati nakati ,sio kwa siri san na sio kwa sauti sana.
- Awe ni mwenye kukiri madhambi yake,na kuomba msamaha, na awe ni mwenye kuzikiri neema za Allah kwake na kutoa shukrani kwa neema hizo.
- Asiwe mwenye kujikalifisha katika maombi yake (Kama kutaka kusoma dua ndefu ndefu,ngumu,asizotambua maana yake n.k).
- Katika kuomba kwake awe na muda mzuri,na aommbe kwa unyenyekevu,na awe
- katika hali ya uoga na pia kujipa matumaini mazuri.
- Kama ana haki za watu azirejeshe na afanye toba ya kweli.
- Katika maombi yake awe mwenye kurudia rudia mara tatu.
- Awe ameelekea Qibla.
- Anyanyue mikono yake wakati wa Dua.
- Kama akiweza kushikaudhu kabla ya maombi itakuwa bora zaidi.
- Awe mwenye adabu wakati anamuomba Allah.
- Mtume Muhammad – sala na salamu zimwendee – amesema

**« Duaa ndio ibada hasa».**

# NA MIONGONI MWA ADABU ZA MAOMBI

- Mwenye kuomba kwanza ajiombee mwenyewe,kisha awaombee na wengine,kwamfano akisema:

*Ewe Mola wangu; Nisamehe na umsamehe na fulani.*

- Amuombe Allah kupitia majina yake mazuri na Sifa zake tukufu, au kupitia matendo yake mazuri aliyoyatenda, au aombe dua ya mtu miongoni mwa waja wema,kwa sharti awe yu hai na yupo naye.
- Ajitahidi chakula chake na kinywaji chake na mavazi yake viwe vya halali.
- Asiombe madhambi au kukata udugu.
- Muombaji awe na sifa ya kuamrisha mema na kukataza mabaya, mwenye kujiepusha na maaswi.

## NYAKATI MUHIMU AMBAZO MAOMBI HUJIBIWA

- Katikati ya Usiku
- Mwisho wa kila swala.
- Baina ya adhana na Iqama.
- Theluthi ya mwisho ya Usiku.
- Wakati inaponadiwa swala za faradhi.
- Wakati mvua inapo nyesha.
- Saa ya mwisho katika siku ya Ijumaa.
- Wakati wa kunywa maji ya Zamzam ikambatana na nia ya kweli.
- Wakati akiwa katika Sijdah.

# NYAKATI MUHIMU AMBAZO MAOMBI HUJIBIWA

- Dua ya muislamu kumuombea ndugu yake muislamu
- Dua ya kuombwa siku ya Arafa
- Pindi Waislamu wanapokutana katika vikao vya kumtaja Allah.
- Dua njema au mbaya ambayo mzazi anamuombea mwanae.
- Dua ya Msafiri
- Dua ya mtoto mwema kuwaombe wazazi wake
- Dua baada ya udhu,pindi anapoomba dua iliyopokewa baada ya udhu.
- Dua baada ya kupiga jamaraati,lile kuta la mwanzo.
- Dua baada ya kupiga jamaraati, kuta la katikati.
- Kuomba dua ndani ya Alkaaba, na mwenye kuswalia ndani ya Hijri Ismail basi huyo anakuwa yuko ndani ya Alkaaba.
- Dua inayoombwa juu ya mlima wa swafaa.
- Dua inayoombwa juu ya Mar-waa.
- Dua inayoombwa pale Mash-aril-haraam (Muzdalifa)

Na bila shaka hakika Muumini anamuomba Mola wake kila wakati na popote anapokuwa na Allah yuko karibu na waja wake.

Allah amesema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ
فَلْيَسْتَجِيبُوا۟ لِى وَلْيُؤْمِنُوا۟ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾ سورة البقرة

***" Na pindi wakikuuliza waja wangu kuhusu mimi waambie niko karibu, najibu maombi ya muombaji pindi anapo niomba, basi na waniitike na waniamini ili wapate kuongokewa"*** .(2:186)

**Lakini nyakati hizi tulizo zitaja na maeneo haya na hali hizi yatakiwa zipewe umuhimu mkubwa zaidi.**

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

Katika Arafa au Muzdalifa na maeneo mengine miongoni mwa maeneo mazuri ya kuomba.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AS-ALUKAL-AFUWA WAL-AAFIYAH, FII DIINII WADUNIYAAYA,WA AHALII WAMAALII. ALLAHUMMASTUR AURAATII, WA AAMIN RAUAATII. ALLAHUMMA IHFADHNII MIN BAINI YADAYYA,WAMIN KHALFII,WA AN YAMIINII WA AN SHIMAALII, WA AUDHU BIADHWAMATIKA AN UGHTAALA MIN TAHTII.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA AAFINII FII BADANII, ALLAHUMMA AAFINII FII SAMUII, ALLAAHUMA AAFINII FII BASWARII LAAILAAHA ILLAA ANTA. ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MINALKUFRI WAL-FAQRI, WAMIN ADHAABIL-QABR, LAAILAAHA ILLAA ANTA. ALLAHUMMA ANTA RABBII LAILAAHA ILLAA ANTA KHALAQTANII WA ANAA ALAA AHDIKA WAWAADIKA MSTATWAATU, AUDHUBIKA MINSHARRI MAASWANAATU, ABUU U LAKA BINIIMATIKA ALAYYA, WA ABUU U BIDHAMBII, FAGHAFIRLII FAINNAHUU LAA YAGHFIRU DHUNUUBA ILLAA ANTA.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNII AUDHUBIKA MINAL-HAMMI WAL-HAZAN, WA AUDHUBIKA MINAL- AJZI WAL-KASAL, WA AUDHUBIKA MINAL BUKHLI WAL JUBNI, WA AUDHUBIKA MIN GHALABATID-DAIN WA QAHARIR-RIJAAL.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMAJ- AL AWWALA HAADHAL-YAUMI SWALAAHAN, WA AUSATWAHUU FALAAHAN, WA AAKHIRAHUU NAJAAHAN. WA AS-ALUKA KHAIRAYID-DUNIYAA WAL-AAKHIRAH, YAA AR-HAMAR-RAAHIMIIN.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNII AS-ALUKAR-RIDHWAA BAADAL-QADHAA , WABARDAL -AISHI BAADAL MAMAATI, WA LADHATAN-NADHWARI ILAA WAJHIKAL-KARIIM, WASHAUQA ILAA LIQAAIKA, FII GHAIRI DHWARRAA`A MUDHWIRRAH, WALAA FITNATIN MUDHWILLAH. WA AUDHUBIKA ANADHLIMA AU UDHLAMA, AU AATADIYA AU YUUTADAA ALAYYA, AU AKSIBA KHATWIIATAN AU DHAMBAN LAA TAGHFIRUHU.

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN AN URADDA ILAA ARDHALIL UMRI. ALLAHUMA IHDINII LIAHSANIL-AAMAAL, WAL- AKHLAAQI , LAA YAHDII LIAHSANIHAA ILLAA ANTA..WASRIF ANNII SAYYIAHAA ,LAA YASRIFU ANNII SAYYIA HAA ILLAA ANTA.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA ASLIH LII DIINII..WAWAS-SII LII FII DAARII..WABAARIK LII FII RIZQII. ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MINAL-QAS-WATI, WALGHAFLATI, WADHULLATI, WALMASKNATI. WA AUDHUBIKA MINAL-KUFRI WALFUSUUQI, WASHIQAAQI, WASUMUATI , WARRIYAAI .WA AUDHUBIKA MINAS-SWAMAMI WAL-BUKMI, WAL JUDHAAMI ,WA SAYYIAL-ASQAAMI .

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA AATII NAFSII TAQUWAAHAA. WAZAKKIHAA ANTA KHAIRU MAN ZAKKAAHA. ANTA WALIYYUHAA WAMAULAAHAA. ALLAAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN ILMIN LAA YANFAU. WAQALBIN LAA YAKHSHAU. WANAFSIN LAA TASHBAU. WA DAAWATIN LAA YUSTAJAABU LAHAA.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MINSHARRI MAA AMILTU ,WAMINSHARRI MAA LAM AAMAL,ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN ZAWAALI NIIMATIKA , WATAHAWWULI AAFIYATIKA, WAFUJAATA NIQMATIKA, WAJAMIIA SAKHTWIKA.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MINAL-HADMI WAT-TARADDII, WAMINAL GHARAQI WALHARAQI, WALHARAMI, WA AUDHUBIKA MIN AN-YATAKHABBATWANII ASHAITWAANI INDAL- MAUTI ,WA AUDHUBIKA MIN AN AMUUTA LADIIGHAN, WA AUDHUBIKA MIN TWAMAIN YAHDII ILAA TWABAIN.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA RABBAS-SAMAAWAATI , WARABBAL -ARDHWI,WARABBAL-ARSHIL -ADHWIIM, RABBUNAA WARABBU KULLI SHAI IN. FAALIQUL-HABBI WAN-NAWAA, MUNZILUT-TAURAATI WAL-INJIIL WALQUR-AANI, AUDHUBIKA MIN KULLI SHAI IN , ANTA AAKHIDHUN BINAASWIYATIHII, ANTAL- AWWALU FALAISA QABLAKA SHAI UN, WA ANTAL- AAKHIRU FALAISA BAADAKASHAI UN, WA ANTADH-DHWAAHIRU FALAISA FAUQAKA SHAI UN, WA ANTAL BAATWINU FALAISA DUUNAKA SHAI UN, IQDHWI ANNII AD-DAINA, WA AGHNINII MINAL-FAQRI .

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN MUNKARAATIL- AKHLAAQI, WAL-AAMAAL, WAL-AHWAAI,WAL-AD-WAAI. WA AUDHUBIKA MIN GHALABATID-DAIN, WQAHRIR-RJAALI, WASHAMAATATIL- AADAI. ALLAAHUMMA ASWILIH LII DIINII, ALLADHII HUWA ISUMATI AMRII, WA ASWILIH LII DUNIYAAYA ALLATII FIIHAA MAASHII, WA ASWILIH LII AAKHIRATII ALLATII ILAIHAA MAADII, WAJ-ALIL-HAYAATA ZIYAADATAN LII FII KULLI KHAIRIN, WAJ-ALIL MAUTA RAAHATAN LII MIN KULLI SHARRI. RABBI AINNII WALAA TUIN ALAYYA. WANSURNII WALAA TANSUR ALAYYAA. WAHDINII WAYASSIRIL HUDAA LII.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMAJ-ALNII DHAKKAARAN LAKA, SHAKKAARAN LAKA, MITUWAA AN LAKA, MUKHBITAN ILAIKA, AWWAAHAN MUNIIBAN. RABBI TAQABBAL TAUBATII,WAGHSIL HAUBATII, WA AJIB DAAWATII, WATHABBIT HUJJATII, WAHDI QALBII, WASADDID LISAANII,WASLUL SAKHIIMATA SWADRII.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNII AS-ALUKA ATHABAATA FIL-AMRI, WAL-AZIIMATA ALAR-RUSHDI, WA AS-ALUKA SHUKRA NIIMATAKA, WAHUSNA IBAADATIKA, WA AS-ALUKA QALBAN SALIIMAN, WALISAANAN SWAADIQAN, WA AS-ALUKA MIN KHAIRI MAA TAALAM, WA AUDHUBIKA MIN SHARRI MAA TAALAM, WA ASTAGHFIRUKA MIMMAAA TAALAM, WA ANTA ALLAAMUL-GHUYUUBI.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA ALHIMNII RUSHDII, WAQINII SHARRA NAFSII. ALLAAHUMMA INNII AS-ALUKA FIILAL-KHAIRAATI, WATRKAL-MUNKARAATI, WAHUBBAL- MASAAKIIN,WA ANTAGHAFIRALII WATR HAMANII, WAIDHAA ARADTA BI IBAADIKA FITNATAN FATAWAFFANII ILAIKA GHAIRA MAFTUUN.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA HUBBAKA ,WAHUBBA MAN YUHIBBUKA, WAHUBBA KULLA AMALIN YUQARRIBUNII ILAA HUBBIKA.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNI AS-ALUKA KHAIRAL-MAS-ALAH, WA KHAIRADDUAA, WA KHAIRAN-NAJAAH, WA KHAIRATH-THAWAABI, WATHABBITNII ,WATHAQIL MAWAAZIINII,WAHAQIQ IIMAANII,WAR-FAA DARAJATII,WATAQABBAL SWALAATII WA IBAADAATII,WAGHFIR KHATWII AATII, WA AS-ALUKAD-DARAJAATIL-ULAA MINALJANNATI.

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNI AS-ALUKA FAWAATIHAL-KHAIRI, WA KHAWAATIMAHUU WAJAWAAMIAHUU, WA AWWALAHUU WA AAKHIRAHUU, WADHWAAHIRAHUU WAABAATWINAHUU, WAD-DARAJAATIL-ULAA MINAL-JANNAH.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA AN TARFAA DHIKRII, WA TADHWAA WIZRII, WA TUTWAHIRA QALBII, WATUHSWINA FARJII , WATGHFIRALII DHAMBII.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA ANTUBAARIKA FII SAMUII ,, WAFII BASWARII, WAFII KHALQII WAFII KHULUQII,WAFII AHALII WAFII MAHYAAYA, WAFII AMALII, WATAQABBAL HASANAATII, WA AS-ALUKAD-DARAJAATIL-ULAA MINALJANNATI.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN JAHDIL BALAAI, WADARAKI SHAQAAI, WASUUUIL-QADHWAAI, WASHAMAATATIL-AADAI. ALLAAHUMMA MUQALLIBAL-QULUUBI THABBIT QALBII ALAA DIINIKA. ALLAHUMMA MUSWAR-RIFAL QULUUBI SWAR-RIF QALBII ALAA TWAATIKA.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA ZIDNAA WALAA TANQUSNAA, WA AKRIMNAA WALAA TUHINNAA, WA AATWINAA WALAA TAHRIMNAA, WA AATHIRNAA WALAA TU`UTHIR ALAINAA. ALLAAHUMMA AHSIN AAQIBATINAA FIL-UMUURIKULLIHAA, WA AJIRNAA MIN KHIZYID-DUNIYAA WA ADHAABAL-AAKHIRA .

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA AQSIM LANAA MIN KHASHIYATIKA MAA TAHUULU BIHII BAINANAA WABAINA MAASWIYATIKA. WAMIN TWAATIKA MAA TUBALLIGHUNA BIHI JANNATAKA, WAMINAL-YAQIINI MAA TUHAWWINU BIHII ALAINAA MASWAAIBAD-DUNIYAA, WAMATTIINA BI ASMAAINAA, WA ABSWAARINAA, WAQUWWAATINAA MAA AHYAITANAA, WAJ-ALHULWAARITHA MINNAA, WAJ-AL THA`ARANA ALAA MAN DHWALAMANAA,WANSURNAA ALAA MAN AADAANAA, WALAA TAJ-ALID-DUNIYAA AKBARA HAMMINAA, WALAA MABLAGHA ILMINAA, WALAA TAJ-AL MUSWIIBATANAA FII DIININAA, WALAA TUSALLIT ALAINAA BIDHUNUUBINAA MAN LAA YAKHAAFUKA WALAA YAR-HAMUNAA.

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNI AS-ALUKA MUUJIBAATI RAHMATIKA, WAAZAAIMA MAGHFIRATIKA, WAL-GHANIIMATA MIN KULLI BIRRI,WAS-SALAAMATA MIN KULLI ITHMI , WALFAUZA BIL-JANNATI , WAN-NAJAATA MINAN-NAAR.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA LAA TADAA LANAA DHAMBAN ILLAA GHAFARTAHU , WALAA AIBAN ILLAA SATARTAHUU, WALAA HAMMAN ILLAA FARRAJ-TAHUU, WALAA DAINAN ILLAA QADHWAITAHUU, WALAA HAAJATAN MIN HAWAIJID-DUNIYAA WAL-AAKHIRATI HIYA LAKA RIDHWAN WA-LANAA FIIHAA SWALAAHAN ILLAA QADHWAITAHAA, YAA AR-HAMAR-RAAHIMIIN. ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA RAHMATAN MIN INDIKA ,TAHDII BIHAA QALBII, WATAJ-MAA BIHAA AMRII, WATALUMMA BIHAA SHAATHII, WATAHFADHWA BIHAA GHAAIBII, WATAR-FAA BIHAA SHAA-HIDII, WATUBAYYIDHWA BIHAA WAJ-HII, WATUZAKKII BIHAA A`MALII, WATALHIMANII BIHAA RUSHDII, WATARUD-DA BIHAL-FITANA ANNII, WATA`ASWIMANI BIHAA MIN-KULLI SUUIN.

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA INNI AS-ALUKAL-FAUZA YAUMAL-QADHWAI, WA A`ISHAS-SUADAAI, WAMANZILA SHUHADAAI, WAMURAAFAQATAL -ANBIYAAI, WAN-NASRA ALAL-AADAAI.

**ALLAHUMMA**

SALLAHUMMA INNI AS-ALUKA SWIHATAN FII IIMANI , WA IIMAANAN FII HUSNI KHULUQIN, WANAJAAHAN YAT-BAUHUU FALAAHUN, WA-RAHMATAN MINKA WA AAFIYATAN MINKA, WAMAGHFIRATAN WA-RIDH-WAANAN. ALLAHUMMA AS-ALUKA SWIHATA WAL-IFFATA, WA-HUSNAL-KHULUQI , WAR-RIDHWAA BIL-QADARI . ALLAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN SHARRI NAFSII, WAMIN SHARRI KULLI DAABBATIN ANTA AAKHIDHUN BINAASWIYATIHAA, INNA RABBII ALAA SWIRAAT-WIN MUSTAQIIM. ALLAHUMMA INNAKA TASMAU KALAAMII, WATARAA MAKAANII , WATAALAMU SIRRII WA ALAANIYATII , WALAA YAKHFAA ALAIKA SHAI-UN MIN AMRII, WA ANAA AL-BAAISUL-FAQIIR, WALMUS-TAGHIITHUL-MUSTAJIIRU, WAL-WAJILUL-MUSHFIQU, ALMUQIRRUL-MUUTARIFU ILAIKA BIDHAMBIHII. AS-ALUKA MAS-ALATAL-MISKIIN, WA ABTAHILU ILAIKA IBTIHAALAL-MUDHNIBU ADHALIIL, WA AD-UUKA DUAALKHAAIFU ADHARIIR, DUAA`A MAN KHADHWAAT LAKA RAQA-BATUHU, WADHALLA LAKA JISMUHU, WARAGHIMA LAKA ANFUHUU.

# DUA AMBAZO ZINANAASIBU KUZIOMBA AU KIASI KITAKACHO KUWEZEKANIA

**ALLAHUMMA**

ALLAHUMMA LAKA ASLAMTU. WABIKA AAMANTU. WA ALAIKA TAWAKKALTU. WA ILAIKA ANABTU, WABIKA KHAASWAMTU. AUUDHU BI IZZATIKA AN TUDHILLANII, LAAILAAHA ILLAA ANTA. ANTAL-HAYYU ALLADHII LA YAMUUTU, WALJINNU WAL-INSU YAMUUTUUN.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA INNII AUDHUBIKA MIN ILMIN LAA YANFAU , WAMIN QALBIN LAA YAKHSHAU, WAMIN NAFSIN LAA TASHBAU, WAMIN DAAWATIN LAA YUSTAJAABU LAHAA.

**ALLAHUMMA**

ALLAAHUMMA JANNIBNII MUNKARAATIL-AKHLAAQI, WAL-AAMAALI, WAL-AHAWAAI, WAL-AD-WAAI. ALLAAHUMMA ALHIMNII RUSHDII WA AIDHNII MIN SHARRI NAFSII. ALLAHUMMA IKFINII BIHALAALIKA A`N HARAAMIKA, WA AGHNINII BIFADHLIKA AMMAN SIWAAKA. ALLAHUMMA INNII AS-ALUKALHUDAA, WATTUQAA , WAL-AFAAFA WALGHINAA. ALLAAHUMMA INNII AS-ALIKAL-HUDAA WAS-SADAADA. ALLAHUMMA INNII AS-ALUKA MINAL-KHAIRI KULLIHII , A`AJILIHII WA AAJILIHI, MAA ALIMTU MINHU WAMAA LAM AALAM, WA AUDHUBIKA MINASHARRI KULLIHI A`AJILIHII WA AAHILIHI, MAA ALIMTU MINHU WAMAA LAM AALAM. WA AS-ALUKA MIN KHAIRI MAA SA-ALAKA MINHU ABDUKA WA NABIYYUKA MUHAMMADIN SWALLALLAAHU ALAIHI WASALLAM, WA AUDHUBIKA MIN SHAR-RI MASTAADHA MINHU ABDUKA WA NABIYYUKA MUHAMMADIN SWALLALLAAHU ALAIHI WASALLAM. ALLAHUMMA INNII AS-ALUKALJANNATA WAMAA QARRABA ILAIHAA MIN QAULIN WA AMAL, WA AUDHUBIKA MINAN-NAARI WAMAA QARRABA ILAIHAA MIN QAULIN WA AMAL,WA AS-ALUKA ANTAJ-ALAKULLA QADHWAIN QADHWAITAHU LII KHAIRAN.

LAAILAAHA ILLALLAAHU WAHDAHU LAA SHARIIKA LAHU LAHUL-MULKU WALAHUL-HAMDU, YUHYII WAYMIITU, BIYADIHILKHAIRU, WAHUWA ALAAKULLI SHAI-IN QADIIRU.

SUBHAANALLAAHI WALHAMDULILAAHI, WALAAILAAHA ILLALLAAHU WALLAAHU AKBARU , WALAAHAULA WALAAQUWWATA ILLAA BILLAAHIL- ALIYYIL-ADHWIIM.

WASWALLALLAAHU ALAA SAYYIDINAA MUHAMMADIN WA-ALAA AALIHII WASWAHBIHII WASALLAMA.

# DUA YA KUPANDA KIPANDWA

**Sa ngalan ng Allah , Ang lahat ng papuri ay nararapat lamang sa Allah**

**Sa ngalan ng Allah , Ang lahat ng papuri ay nararapat lamang sa Allah**

**“ ANG KABANALAN AY SA ALLAH NA LUMIKHA DITO SA ATIN , NA DI NATIN KAYA NGUNIT GUSTO NIYA , TUNAY NA SA PANGINOON TAYO BABALIK “**

Bismillah, elhamdulillah

سُبْحَٰنَ ٱلَّذِى سَخَّرَ لَنَا هَٰذَا وَمَا كُنَّا لَهُۥ مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾ وَإِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنقَلِبُونَ ﴿١٤﴾

Kisha anasema: ALHAMDU LILAAHI , ALHAMDULILAAHI , ALHAMDULILAAHI. ALLAAHU AKBARU , ALLAAHU AKBARU , ALLAAHU AKBARU, SUBHAANAKA ALLAAHUMMA INNII DHWALAMTU NAFSII, FAGHFIR-LII, FA INNAHUU LAA YAGHAFIRU DHUNUUBA ILLAA ANTA.

## DU YA SAFARI

Allahu akbar allahu akbar allahu akbar “

سُبْحَٰنَ ٱلَّذِى سَخَّرَ لَنَا هَٰذَا وَمَا كُنَّا لَهُۥ مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾ وَإِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنقَلِبُونَ ﴿١٤﴾

Allahuma inna nasaluka fii safarina hadha albira wattaqwa waminal-amali ma tardha allahuma hawin alaina safarana hadha watwi anna buudahu , allahuma anta swahibu fisafar walkhalifatu filahli, allahuma inni audhu bika min waathai safari wakaabatin manthari wasuuil mun-qalabi filmali waahli, na akirejeya atasoma duaa hii hii na atazidisha maneno haya: aaibuna taaibuna aabiduna lirabina hamidun.

## DUA INAYOOMBWA KATI YA RUKNUL-YAMAAN NA HAJARUL-ASWAD

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾

**RABBANAA AATINAA FID-DUNIYAA HASANATAN ,WAFIL-AAKHIRATI HASANATAN, WAQINAA ADHAABAN-NAAR.**

۞ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ

**DUA YA KUOMBWA JUU YA SWAFAA NA MARUWAA**

**Mtume alipokaribia safa akasoma**

Kisha akasema na anza kama alivio anza Allah..

Alianza na safa .. Alipanda juu yam lima wa safa mpaka akaiona Alkabah akaelekea Qiblah, akampwekesha Allah na kumtukuza akasema: Lailaha ila Allah wahdahu la sharika lahu lahul mulku walahul hamdu wahuwa ala kuli shaiin qadir, Laiha ilallahu wahdahu, anjaza waadahu, wanaswara abdahu, wahazamalahzaba wahdahu. Kisha akaomba baina yake. Alisema mfano wa maneno hayo mara tatu na akafanya alipofika marwah kama aliyofanya alipokuwa safa.

# EWE NDUGU YANGU ULIEKUJA KATIKA HIJJAH

Ewe uliekuja kutoka sehemu ya mbali na juu ya kipandwa kilicho choka kutokana na ummbali wa safari,kwahakika inakupasa ujitahidi saana kuilinda Hijja yako,kutokana na madhambi,na maovu ,mijadala,maaswi. Na Hijjah yako iwe yenye kuafikiana na mafundisho yaliyokuja katika kitabu kitukufu, na katika Sunna za Mtume – Sala na salamu zimwendee- na iwe kwa namna ambayo ni kamilifu,ili upate malipo makubwa, kusamehewa madhambi,kufutiwa makosa,kunyanyuliwa daraja, na kuipata Pepo kwa fadhla za Allah na Rehma zake, na hiyo ndiyo Hijjah Mabruur..

Maana Hijjah ambayo ni Mabruur ambayo malipo yake ni Jannah, ni ile Hijja ambayo hukumu zake zimetimizwa, na ikatekelezwa kikamilifu, isiyokuwa na mahambi ndani yake, iliyopambwa na matendo mema na kheri mbalimbali.

Wamesema wanahcuoni kwamba : Ni ile ambayo mtekelezaji hakumuasi Allah katika ibada yake hiyo.

Kwahiyo tunaiusia nafsi yako yenye imani ijitahidi kushikamana na kitabu cha Allah, na kumuiga Mtume -sala na salamu zimwendee-na uwe ni mfano wa kuigwa kwa wale walioko karibu yako, katika kusaidiana na ndugu zako Mahujaji,ili Hija yako iwe ni Mabruur, na juhudi zako ziwe zenye kushukuriwa...Na urejee kwa watu wako ukiwa huna madhambi kama siku uliyozaliwa na mama yako..msafi kabisa huna uchafu,ukiwa umesamehewa..na pindi utakapo rudi Nchini kwako ,kila wakati ambapo nafsi yako itakulingania kufanya madhambi....

Kumbuka wakati ulipokuwa unatufu katika Alkaaba, unakwenda baina ya Swafa na Maruwa.

Kumbuka siku uliposimama katika uwanja wa Arafa ilihali umenyanyua mikono yako ukitaraji Rehma za Allah na msamaha wake.

Kufanya hivyoo bilashaka kutakusaidia kuyaepuka madhambi na maaswi.

Tunawaombea kwa Allah Mahujaji wote awajaalie Hajji ambayo ni Mabruur, na juhudi zenye kushukuriwa ,hakika Yeye ni muweza wa kila kitu.

Sala na salamu zimwendee Mtume wetu Muhammad ,na

ahli wake na Maswahaba wake wote.

***Talal Ahmad Alaqeel***

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1 | Miongoni mwa adabu za Safari | 8 |
| 2 | Miiqaati za kuhirimia | 10 |
| 3 | Kuhirimia | 12 |
| 4 | Yaliyo katazwa kuyafanya baada ya kuhirimia | 14 |
| 5 | Fafanuzi wa Nusuki | 17 |
| 6 | Namna ya utekelezaji wa Umrah | 19 |
| 7 | Namna ya utekelezaji wa Hijjah | 27 |
| 8 | Tarehe nane ya mwezi wa Dhulhijjah | 28 |
| 9 | Arehe tisa ya mwezi wa Dhulhijjah. | 30 |
| 10 | Muzdalifa | 32 |
| 11 | Tarehe kumi ya mwezi wa Dhulhijjah | 34 |
| 12 | Twawaaful-ifaadhwa | 36 |
| 13 | Masiku ya Tashriiq | 37 |
| 14 | Twawafu ya kuaga | 39 |
| 15 | Nguzo na wajibu za Hijjah | 40 |
| 16 | Hukmu zinazo muhusu mwanamke muumini | 41 |
| 17 | Namna ya kufanya ziara katika Msikiti wa Mtume | 47 |
| 18 | Fatwa muhimu | 53 |
| 19 | Dua | 67 |

لغة سـواحيليـة

Mamlaka ya Kiarabu ya Saudia-

وزارة الشؤون الإسلامية والدعوة والإرشاد

We propagate and clarify extensively issues related to hajj in many languages and through practical ways.

www.al-islam.com
www.qurancomplex.com

رقم الإيداع : ٢٣/٣٩١٧٠
ردمك : ٩٩٦٠-٤١-٩٦٤-٩